

CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION

(CKRC)

VERBATIM REPORT OF

CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS,

CHERANGANI CONSTITUENCY, HELD

AT ST. ANDREWS CHURCH

ON

Thursday 27th June, 2002

CONSTITUENCY PUBLIC HEARING CHERANGANI CONSTITUENCY –
THURSDAY 27TH JUNE 2002 AT ST. ANDREWS CHURCH

Present:

Com. Dr. Mosonik arap Korir
Com. Dr. Charles Maranga

Secretariat:

Hasan Mohamed - Programme Officer
Anne Cheron - Assistant Programme Officer
Susan Mutile - Verbatim Recorder

The meeting started at 10.00 a.m, with a prayer by Leah Kimani and Commissioner Mosinik in the chair.

District Coordinator: Mliofika na wale ambao bado hawajafika, tungeomba mfike ili muweze kutoa maoni yenu. Kabla ya kuanza shughuli rasmi, nitauliza mama atuongoze kwa maombi kisha tutawajulisha wageni waliopo hapa, halafu ndipo mtaanza kutoa maoni, mama karibu.

Leya Kimani: Tutasimama ili tuweze kumshukuru Mungu, na kwa majina naitwa Leya Kimani, ni msimamizi wa hili kanisa la St. Andrews, na hivyo mnakaribishwa sana mjisikie mkiwa huru, ili mkaweze kutoa maoni yenu, tukasaidie nchi yetu ya Kenya, na tuombe.

Baba mwenyezi na mwenye rehema tunanyenyekea chini ya miguu yako wakati huu, tukiomba nguvu zitokazo kwako juu mbinguni ili zikaweze kutuongoza wakati ambapo tunatoa maoni yetu kwa ajili ya Katiba ya nchi yetu. Tunajua ya kwamba Mungu baba unajua yote ambayo tunahitaji, na tunaamini ya kwamba utatusaidia kutoa yale ambaye yatajenga nchi yetu. Tunataka kukushukuru kwa wageni wetu ambaye wametoka mbali, na commissioners na ma-lawyers, na hata wale wanao wanasimamia kazi hii yote Mungu wetu ukazidi kuwapa nguvu zitikazo kwako juu mbinguni, ukazidi kuwapa hekima itokayo kwako juu mbinguni, ili wanapoendea kufanya kazi hii, ikaweze kufanikiwa. Tunajua Mungu unajua mwanzo wa kila jambo, na utanza nasi, utaenenda nasi, na hata utamalizia nasi, na utukufu wote wa kazi hii ikurudie eee wewe baba yetu, na ni katika jina safi ya Yesu Kristo aliye bwana na mwokozi wetu.

Audience: Amen.

Leya Kimani: Asanteni.

District Coordinator: Asante sana. Ningependa kuchukua nafasi hii kuwafahamisha badhi ya wanakamati, katika kamati ya eneo ya Charangani. The Committee Members tafadhali simama ili wajue. Tuko na wanakamati wengi, wengine tumewahusisha katika sehemu zingine wanatusaidia kwa hivyo ningewauliza wataje wajina yao.

Okull: Hamjambo nyote?

Audience: Hatujambo.

Okull: Bwana commissioners na wote wa Cerangani Sibanga, mimi nimesimama hapa ni Mama Naomi Okull, na ninasimamia upande wa Saboti Constituency, lakini nimekuja kusaidia leo Cherangani, hawa wenzangu. Asanteni.

Joseph Chebii: Hamjamboni wote? Mimi kwa manjina ni Joseph Chebii na ninawakilisha Honourable Zipporah Kittony nikiwa hapa. Ninataka niseme karibuni commissioners wote na wananchi karibuni hapa.

Nyambane: Hamjamboni wote, kwa majina ni Mary Nyambane, mwana kamati Saboti Constituency lakini leo tumekuja kufanya kazi hapa Cherangani. Asante.

District Coordinator: Kwa hivyo karibuni, kuna watu wetu wengi ambao tumewahusisha katika kazi hapa nje. Kuna mzee

Siwa ambaye ni mwana kamati, kuna Binti Sarah Kogo ambaye ni mwana kamati eneo hili, kuna Councillor Kengasia ambaye ni mwana kamati, na wengine. Tumewahusisha katika na kazi hapa na pale, lakini watakupepo siku inapoendelea. kwa nafsi hi ningelipenda kuwpatia commissioners, najua kila mtu anashangaa na kutizama, anaajiuliza ni nani. Wacha nimpe nafasi ya kujitambulisha, na kututambulishia wale wageni ambaye wamekuja na yeye lakini kabla hapo, bwana commissioners feel very welcome, watu wa Cherangani ni watu wazuri sana, kwa hivyo uswe na wasiwasi, usiwe na hofi yoyote ile, welcome sir.

Com. Dr. Monik Korir: Hamjambo watu wa Cherangani?

Audience: Hatujambo.

Com. Dr. Monik Korir: Vile Bwana District Co-ordinator amesema nimeanza kujisikia kama siko nyumbani. Sijapata wakati mwingine kufika area hii, nimefika tu town nikipita kwa barabara. Nimeona nchi imekaa vizuri na ninahakika kwamba tutaitifanya kazi vizuri. Kwanza kabisa mimi ni Commissioner Dr. Mosonik arap Korir. Najua kwamba ma-commissioner wako area hii yenu.

Tuko kwa pannels nane, tumejigawanya kila panel ina commissioners watatu. Tukiwa hapa, wengine wenzetu wako Turkana North, Turkana North Tena, Central, Kapenguria, kwanzia Mosop na Marakwet West, watu watatu watatu. Nilitakiwa niwe hapa na wenzangu wawili wengne. Mmoja ni Bibi Peter Aaroni, ambaye ni makamu wa mwenye kiti ama naibu. Lakini yeye hajaweza kufika kwa ajili mtoto akagojeka, hatafika. Lakini commissioner wa pili mwenzangu ambaye atafika, ni Dr.Charles Maranga. Alikuwa anatoka Nairobi gari ikaharibikia Eldoret. Tunatarajia ataingia kabla ya saa tano.

Nimesoma mimi ni Commissioner Dr. Mosonik arap Kori, niko hapa na mwenzangu kutoka tume ya marekebisho ya Katiba ya Kenya ama C.K.R.C. Wa kwanza kabisa ni Programme Officer Mr. Hassan Mohammed, yeye yuko hapa, halafu naibu wae ni Miss Anne Kwamucho ambaye ameketi hapa, na wa tatu ambaye ameketi kwa corner ni Miss Susan Mutile, yeye ni Verbatim Recorder. Tukiwa hapa tunayasikiza maoni yenu na ku-record. Mtakuwa mkiniona hapa nikiandika wakati wowote. Mitambo hii inanasa sauti zenu na maoni yenu, na tena Susan kwenye corner atakuwa anarecordi, anaandika na mkono na tena inaingia kwa mashini, ndio badaye aitoe kabisa repoti kamili na hio inaitwa Verbatim recording.

Tukiwa tunaifanya hii kazi, tunafanya kwa njia mbili . Nikutoa maoni kwa njia mbili. Utoe maoni ukiwa umeandika hayo maoni, inaitwa ukiwa na memorandum au written submission, ukisema Kingereza, ukiwa umeandika maoni tunawapa, ama tnakupa dakika tano, tukielewa kwamba yote yameandikwa na tutaenda na kuyasoma. Itasomwa Nairobi kuna secretariat wanasoma na ku- is called to decipher. Kwa hivyo kakika tano ukipwewa sio ya kusoma memorandum kuanzia mwanzo mpaka mwisho, ni kusema ni ku-highlight meaning the most important points, na kufafanua. Njia ya pili, ni kutoa maoni ukiwa hujayaandika, na ukiwa unatoa maoni ambayo ujayaandika inaitwa oral submission ama verbal presentation. Wakati ule tutawapa, ama tutakupa dakika kumi. Ikiwa ujaandika dakika kumi. Ukiwa umeandikia dakika tano. Lugha tutatumiani lugha

mbili rasmi. Kingereza au Kiswahili. Ukiwa unasema, unasema ndio commission iyelewe mambo yako, yaani usemi kwa raia wenzako. kwa hivyo ukijua Kingereza sema straight away, kama lugha za area hii ingiwa tumesikia kwamba constituency ni cosmopolitan. Ukiwa unataka kusema na lugha ingine utueleze mapema, kwamba tuseme kikalenjin, kikuyu ama kitu, na tutajaribu kupata mtu wa kutafsir. Lakini ingesaidia kwa muda na ksa kuelewa direct kama ungesema kwa Kiswahili au Kingereza. Sijui kama tuna sign language interpreter.

Interjection: (not clear).

Com. Dr. Monik Korir: Sasa hatukuja na sign language interpreter kwa ajili, kwa hivyo, kama kuna mtu ambaye aneshida, hasikii, tuelezwe ndio tujaribu kumtafuta huyo mtu wa kutafsiri. Ma-commissioners wana haki ya kuuliza maswala ukiwa unapeana maoni. Maswala ya kufafanua. yaani unaweza kusema kiti na haeleweki sana, na tukiuliza maswala ama swala, usifikirie ni kushindna na wewe, ni kufafanua tuu, na ukiwa hujafikiria usijaribu kufikira, na kwanza kutunga, ama kujilazimisha kujibu. Useme vile nimesema hio ni sawa.

Kila mtu atajiandikisha kwa kikaratasi hiki, na tutaifuata ile orodha iko hapa. Vile watu walikuja, ndio tutawasikiza. Lakini wakati mwingine pengine tutaruka kidogo, tukiona tunatumia tuu akili yetu, tunaona pengine kuna a disabled person, we should not stay here very long, ama kuna wanafunzi wa shule, ama walimu tunaweza kuruka kidogo. Lakini tutaifuata kawaida orodha hii. Mtu akitoa maoni anaketi upande ule mwingine, n kusema kwa microphone, na akisema ataje jina lake tena. Nitaita Samuel Mbugua kwa mfanano wa kwanza hapa. Aje lakini arudie jina, ndio hio jina ingie kwa mashini, na kama unasema kwa niaba yako usema, personal views. Kama kwa niaba ya group utasema tena, halafu mwishowe una-recordi,. Kuna register hapa, pale pale tu tuna record na kuna maswali utaulizwa, anwani na vitu kama hivyo, kwa ajili maoni ya leo ni maoni ya wananchi wa Cherangani. Ikiwa kuna mtu mwingine amepitapita anapita kuwa observer, lakini tunataka maoni ya hapa. Kwa hivyo tunataka tena tuwe na anwani, na hio anwani tena ndio tutaiandika baadaye tukitoa ripoti ya tume, itakuwa ina-report kila mtu ambaye alifika hapa, na jina na anwani.

Kuna watu wengine ambao watakuja, na hawataki kutoa maoni, lakini hata wao wajiandikishe, kwa ajili mwishoe tutasema tulikuwako Cherangani Maili Nane Church, na wananchi ambao walijitokeza kwa kazi hii, walikuwa ni kiasi hiki, watu kama mia mbili. Wale waliosema walikuwa ni hii nambari. Kwa hivyo hata kama hutoi maoni, utajiandikisha tuu ndio iwe kwa record. I think I have said everything that needs to be said. Sasa, is it okay? Sasa tutaanza na mtu wa kwanza kabisa ni Mr Samuel Mbugua (SDA Peace).

Pastor Samuel Mbugua: Testing, Jina langu ni Pastor Samuel Mbugua, ninawakilisha SDA Church, na pia nina maoni yangu binafsi. Kwanza kabisa nataka kuwashukuru tume hii ya uchaguzi na hasa commissioner ambaye mumekuja hapa Cherangani. Mumekuja kwa wakati mzuri. Bwana awabariki na mtakapoenda pengine mwende salama pia. Hivyo basi nataka kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa nafasi hii, maana anafahamu mambo ya Katiba ni kitu cha muhimu, na pia ndani ya bibilia pia mwenezi

Mungu ameweza kuelezea ya kwamba, juu ya wajibu wa serikali, ni kama mkono wake ya kutimiza malengo yake.

Hivyo basi maoni ambayo ningependa kuyatoa kwa ajili ya kikundi hiki, namba moja ni kwamba sisi kama kikundi tunaona ya kwamba kitu cha kwanza kuwe na tofauti ya serikali na dini. Serikali na dini ziwe vitu viwili tofauti. Kusiwe na dini ya serikali.

Jambo lingine ambalo ningependa kutoa kwa kifupi pia, ni uhuru wa kuabudu. Tunatoa maoni ya kwamba, kila mmoja awe na uhuru wa kumwabudu mwenyezi Mungu sawasawa na jinzi mawazo yake inavyomwelezea. Hii iko ni kwamba kil ammoja amuabudu mwenyezi Mungu bila kulazimishwa. Kusiwe nakulazimishwa, ufuata mambo fulani, lakini iwe vile conscience yako inakuambia uweze kumwabudu mwenyezi Mungu. Na jambo lingine pia ambalo ningependa kulisema ni kwamba tungependa pia uhuru zaidi wa kuhubiri. Mtu ajieleze bila kuwa na mpaka ya kwamba labda wewe ni mtu wa dini gani ama dhehebu fulani. Kusiwe na hizo vikwazo za mambo ya kujieleza.

Jambo lingine pia katika hali hio nimeelezea ni uhuru huo wa kumwabudu mwenyezi Mungu na pia tunasema ya kwamba kuwe na uhuru, kusiwe na hii tunaia discrimination (ubaguzi). Either kwa sababu ya umri wako, ama kwa sababu ya dini yako, ama kwa sababu labda ya kabila lako. Hii tunasema ya kwamba kuweze kuwa na uhuru , na kila mtu awe na uhuru licha ya kwamba ni wa dini gani ama ni wa mambo fulani, hayo yote yawe hivi.

Jambo lingine uhuru huo pia, tunasema upatikane kwa wanafunzi, kwa walimu, na hata kwa askari ama wanajeshi. Huu uhuru ambao nazungumzia ni uhuru wa kumwabudu mwenyezi Mungu. Kila mmoja aweze kuwa na uhuru wake wa kumwabudu mwenyezi Mungu, na tunasema ya kwamba katika uhuru huu, wa kumwabudu mwenyezi Mungu, tungependa iweze kuwa clear kwa sababu mara nyingi tunapata matatizo maka kikundi, tunao mwabudu mwenyezi Mungu siku ambayo tunayomwabudu mwenyezi Mungu ya Sabato, ambayo ni Jumamosi mara mingi tunapata vikwazo vingi. Kwa hivyo turatoa mawazo yetu kwa tume hii ya uchaguzi ya kwamba iwe walimu, iwe wanafunzi, iwe wanajeshi ama police, wawe na uhuru ule kama watu binafsi.

Jambo lingine ambalo pia nifikiria hapo nimeelezea kama vile imekua recorded katika Maandiko matakatifu kutoka ishirini nane mpaka kumi na moja, na Luka nne aya ya kumi na sita.

Jambo lingine ni human rights: Tuna advocate ama tunasema ya kwamba kuweze kuwa na uhuru wa, sijui nitasema human rights nafikiri inaeleweka vizuri lakini kwamba, serikali iweze kuwatunza raia wake, iweze kuwakinga. They should be able to take care or to protect the citizen, na hio pia katika maandiko matakatifu Mungu ndio wa kwanza kutoa sheria hio ndani ya mandiko kitabu cha bibilia takatifu.

Jambo lingine pia mambo ya mahakama: Mambo ya mahakama, there should be effective judiciary remedy. Mahakama iweze kuwa huru kama vile maandiko matakatifu yanavyoelezea pia katika kutoka ishirini sita. Mahakama yasiwe mahakama yanayoingiliwa na serikali, ama watu wenye uwezo, na labda mahakama inashurutishwa kwenda direction fulani. Kwa hivyo

tunasema ya kwamba mahakama iweze kuwa huru kuweza kutoa mamuzi,na pia hapa katika mahakama, tunasema ya kwamba tungependa kuna sheria ambayo labda kwa makosa fulani mtu anakatiw kinonga ama kuuwawa.

Sisi tuna-advocate tunasema ya kwamba, badala ya mtu kunyongwa afungwe maisha kwa nin nieleze? Ni kwa sababu, mtu anapofungwa maisha ana nafasi ya kurekebeshwa. Either kama ni mtu aliyekuwa si mcha Mungu kuna nafasi may be kwa sababy ya wale chaplain ambayo wako katika sehemu zile wanaweza kufanya abadilike na pia awe raia mwema wa ufalme wa binguni. Hivyo tunasema sheria ho ya kunyonga ingebadilishwa na badala yake iwe kufungwa maisha. Na katika hali hio ya mambo ya kufungwa, pia watu hawa wangepewa haki zao, maana mimi ninapofungwa jamii yangu imebaki, may be nimefungwa miaka kumi na zaidi, nakua ya kwamba pia hio inaleta, wakati nitatoka labda italeta matatize labda nitakuta watoto wamezaliwa kule. Ingekuwa bora kama kungekuwa hio uhuru ya hawa watu wanaweze kukutana.

Namba ya kwanza tutakuwa tunakinga ukimwi, hata ukimwi unaoangamiza wafungwa. Wanafungwa kule wanatoka kama wamepata ukimwi, may be kama serikali, ama sisi kama raia tuko concerned hio tunaweza kuiepusa, na tukiwa katika sehemu hio pia, tunasema ya kwamba mtu asilazimishwe kuchukua kiapo kinyume na conscience yake. May be imani yako haikuruhusu kuchukua kiapo fulani, mtu Katiba yetu ingeweza kuweka nafasi hio ya mtu ambaye si lazima atoe kiapo kile, aruhusiwe awe namna hio. Na pia jambo lingine tunasema ni kwamba, wazazi wawe na uhuru. Katiba yetu iruhusu wazazi wanaweza kuadhibu watoto wao. Maana mandiko matakatifu yanaeleza vizuri sana katika kitabi cha Methali ya kwamba mzazi asimnyime mtoto kiboko, maana akimpa kiboko atamwoko na mauti. Hivyo Katiba yetu iruhusu, mimi kama mzazi nimuadhibu mtoto wangu. Isiwe ya kwamba nikiwadhibu mtoto ni mambo mengine.

Pia tungependa kusema kuhusu hawa working class. Watu wanaofamilia ambao wanafaanya kazi. Serikali iangalie inapoenda kuwaa transfer. Isiwe ya kwamba, labda mwanamke anapewa transfer Mombasa, mwanaume yuko Nairobi ama mahali fulani, I consider mahali hapo, yaezekana mke wangu anafanya kwa company fulani, ambaye nikipewa transfer kwenda Narobi hio company haipo Nairobi. Basi serikali iangalie kama mimi mwanaume ndio mtende kazi ya serikali, basi nipelekwe transfer karibu na company hio ili nikuwe karibu na mke wangu. Hii tunasema kwa sababu ya mambo ya ukimwi vile mbavyo imekuwa kwa hali ya juu. Tungependa jambo hili tuweze kuliangalia.

Mambo ya childs abuse: Child's abuse tunaizungumzia tukisema ya kwamba watoto, abuse ya kuajiri watoto wadogo under age, either kwa military, ama mahali fulani, katiba yetu iweze kupeana nafasi ya watoto wasiweze kuajiriwa katika hali hio. Mambo ya kutahiri watoto wasichana, pia sisi kama kanisa tunasema ya kwamba isiruhusiwe. Katiba yetu isikubali, kwa sababu ya matatizo ambayo hupatikana.

Jambo lingine ambayo tunalizungumzia ni kwamba, bible ni very clear ya kwamba katika Wekeso tano ishimi na tatu mpaka ishimi na tatu, mwanaume ni kichwa cha nyumba, hivyo kwa kumweshimu mwenyezi Mungu tunazingatia ya kwamba, ile equality sipigi, lakini equalityhio ni katika hali zile zingine zote. Lakini kwa mambo ya kifamilia, kichwa cha nyumba kama mume

ungalipo yeye ni kichwa cha nyumba.

Katiba yetu tungependa iwalinde wachache. Isiwe kwa sababu watu ni wachache, either ni watu wa imani fulani si wengi hivyo wanathalilisa, Katiba haiwatambui, hivyo tunasema Katiba ilinde wachache. Either kabila kama ni chache ama dini ni wachache, hio Katiba yetu iweze kupeana hio nafasi ya kulinda.

Na pia tunasema juu ya General Election, parliamentary: Hii tungeomba ya kwamba Katiba isinyime watu fulani haki yao. Hii inamaanisha ya kwamba wakati mwingine, uchaguzi huu unafanyika situ ya sabato, na kuna wamini wanao pumzika siku ya sabato, na wangependa kumwabdu mwenyezi Mungu, hivyo wananyimwa haki yao. Mfano mzuri ni kwanza, constituency uchaguzi wake, by-election ilifanyika siku ya Jumamosi, mbpo wengine ambao pi wan haki ya ya kupiga kura, hio haki walinyimwa. Taveta mahali fulani pia ilikuwa hivyo, hizo ni mifano fulani. Kwa hivyo tunaomba Katiba yetu iheshimu imani za watu fulani, either hata Jumapili isiweke, maana kuna waumini ambao wanaoenda kanisani Jumapili, watakuwa wamenyimwa ile haki. Iwekwe week days. Mambo ya uchuguzi yote iwekwe week days, ili kila mtu awe na haki ya ku-participate ama kuweza kuchangia.

Pia harambee pia zinapofanyika siku hio hio ya sabato mbayo ni Jumamosi kama ilivyo recorded katika mandiko mtakatifu, pia sisi ni badhi ya community ambao tungependa kupeana michango yetu. Lakini tutashangaa ya kwamba siku hio tunaenda kanisa, lakini harambee inawekwa area yetu. Hivyo serikali ama umma inaweza kutolew vibaya kwamba sisi ni anti-maendeleo. Lakini pia tungependa kuwa katika maendeleo yale, ni harambee hizo ziwewe week days. Pia waoto nimeweze kuelezea kwamba waweze kupewa uhuru ule wa kuabudu katika shule. Katiba yetu iheshimu, iwe clear vizuri ya kwamba kuna uhuru wa kuabudu uwe mwislmu, uwe mkristo, we dini gani, hio Katiba yetu ipeane heshima kwa watu hawa, Ili kusewe watu fulani, ama kikundi fulani kimeweza kufinywa ambacho hakitambulwi na Katiba.

Kitu kingine ambayo tunasema pia ni kuhusu mambo ya ukulima. Serikali iweze kuangalia juu ya wakulima, kwa mfano, kama sisi watu wa Cherangani tunalima mahindi. Tunayalima tunakosa mahali pa kuyauza, kwa hivyo tungependa, tunasema ya kwamba, serikali iweze kutafutia akulima market ya kuuza mimea yao, ama kuweza kuuza nafaka yao, na hata hivyo tunasema juu ya mazingara.

Tunasema mazingara yaweze kulindwa, mazingara, kama forest ziweze kulindwa, na ikiwa serikali itapena mashamba basi iangalie wahitaji. Iangalie maskini ni kina nani. Isiwe wale wanauwezo, na wana mashamba ndio bado tena wanapew mashamba yale. Hivyo inakuwa ya kwamba yule maskini anabaki, maskini hatambuliki. Hio ndio kitu ambayo tunasema na pia tuna-advoate serikali ya umoja, hatuungi majimbo. Tunasema isiwe majimbo, lakini iwezekuwa serikari ya pamoja bila kuwa na majimbo. Nimejaribu kusema kwa kifupi ambaye ni written, mengine yako ndani mtayaandalia na hayo ndio yale ambayo yako written, na ningependa kuongeza sasa kusema ambayo si written.

Com. Mosonik Korir: Now, lakini,

Pastor Samuel Mbugua: Yes thankyou.

Com. Dr. Monik Korir: Umechukua sasa karibu dakika kumi na tano.

Pastor Samuel Mbugua: Nilikuwa nimesema niko mimi pekee yake na pia kuna ya group. Sijui kama nitarudiwa mimi tena?

Com. Dr. Monik Korir: Tuyasikize, sasa ni ya group ama ni yako?

Pastor Samuel Mbugua: Ya group nimemaliza in written.

Com. Dr. Monik Korir: Okay dakika tatu, please maliza haraka.

Pastor Samuel Mbugua: Thank you. Asante. Basi jambo ambalo pia ningelipenda kulisema ni kwamba, ni juu ya mambo ya urais. Rais anapochaguliwa, awezikuwa mtu anayeelewa mambo ya uchumi, ili kuweza kuokoa uchumi katika Kenya nch yetu. Hayo ndio maoni yangu kuhusu upande huo, na jambo lingine ambayo ningependa kusema ni kwamba tungependea Katiba yetu ipeana uhuru zaidi wa mtu kulieleza. Hivi kwamba, nikiwa mimi nina mambo ya kueleza nieleze, na ikiwa basi hayo maoni si hivyo malivyo, mtu mwingine anaweza kuja naye aelee yake, lakini isiwe sa ile labda nimeweka mkutano, ninakuja, serikali inakuja kubomoa ule mkutano. Hio ndio jambo ambayo tungependa kusema. Nipenda kuyasema mimi ya kwamba niwe na uwezo ya kueleza mambo yangu, niwe na uhuru kabisa ninaweza kueleza wakati wowote, mradi serikali isiingilie kuja kufuta mabo yale. Basi kwa sababu ya muda wangu nataka kuachia hapo, na nataka kushukuru sana.

Com. Mosonik Korir: Nikulize tu swala moja

Pastor Simon Mbugua: Thank you.

Com. Mosonik Korir: Ukasema sabato kusemwa na vikwazo vingi. Ningependa kukuliza hii swala ya siku ya kufanya kazi. unajua Jumapili watu hawafanyi kazi.

Pastor Simon Mbugua: Yes.

Com. Mosonik Korir: Jambo lingine tumesikia watu wakisema hata Sabbath day should be just like Sunday in other words, siki ya kutofanya kazi, sijui maoni yako ni yapi?

Pastor Simon Mbugua: yes, maoni yetu ni kwamba, katika bibilia ni clear vizuri kuhusu siku hii ni ya sabato kama vile iko kwa maandiko iweze kuwa siku ambao ni ya kupumzika, na kama haiwezikuwa ni ya kupumzika hapo nataka kusema wale ya kwamba wale waumini wa wakati huo wasiteswe katika sehemu zao za kazi ama wanafunzi wanafukuzwa shule kwa sababu hawakuhudhuria siku hio ya Jumamosi. Katiba yetu ipeane uhuru ya mtu huo.

Com. Mosonik Korir: Asante sana tumsikizie Simon Gitwere ama, tafadhali please.

Simon Twere: Kwa majina naitwa Simon Shikuku Twere

Com. Mosonik Korir: Endelea (not clear)

Simon Twere: Kwa hivyo niko hapa kwa niaba ya Transzoia Squatters Alliance, na nitatoa maoni yangu kufuatana na hii Transzoia's Squatters alliance na yafuatayo ni maoni ya wanachama wa kikundi cha Transzoia's squatters alliance ambacho kinajumlisha vikundi kumi na nne vya ma-squatters, na haya ndio tunapendekeza kwa tume ya kurekebisha Katiba.

Ya kwanza ni kwamba mashamba makubwa yapunguzwe ili kila mtu anayemiliki ekari za juu sana ziwe ekari hamsini, na ile ya chini iwe ekari kumi.

Ya pili ni kwamba, uwezo wa ugawaji wa ardhi uondolewe kwa ofisi ya Rais na mashamba yarudi kwa kamati maalum ambayo imechaguliwa na wananchi kwa ngazi za mashinani, na ni wale ambao hawana mashamba, yaani squatters commission.

Ya tatu ni kwamba sheria ya lease ipigwe marufuku ili mashamba haya yarudi kwa mkamati ya wilaya kwa minajili ya wale wasio na makao.

Ya nne ni kwamba vijana wa kiume na wakike pia wakumbukwe wakati pia wakumbukwe wakati wa ugawaji wa ardhi kote nchini.

Ya tano ni kwamba, mashamba yale ambayo yalinyakuliwa yatambuliwe kote nchini hasa Transzoia, na yarudishwe kwa kamati ya wilaya, na wanyakuzi wote wasititakiwe, na ardhi hio irudie wenyewe.

Ya sita ni kwamba, mashamba ya KARI cases, yale ambaye yalinyakuliwa, na yale bado, yatambuliwe, na yahifadhiwe kwa minajili iliyotengewa.

Ya saba ni kwamba, mashamba yote yanayokaliwa na yatumiwi kwa usalishaji yatozwe ushuru wa juu, kwa minajili ya usalishaji kwa watu wa eneo hiyo ama wilaya hio.

Ya nane ni kwamba, katika ugawaji wa ardhi, kusiweko mambo ya ukabila, kwa mfano eti shamba hili ni la Saboat, ama Bukusu, ama Nandi.

Ya tisa ni kwamba Mbuga za wanyama wa pori zipunguzwe ili wanyama watengewe sehemu ndogo, na wale wasio na mashamba wapewe sehemu iliyosalia.

Ya kumi ni kwamba, masorofea wa kibinafsi, yaani private surveyors, wondolewe kwa kupima mashamba, na badala yake masorofea wa serikali waachiwe kazi hio, na wapime na kibali kutoka kwa tume hii ya masquatters wakishiriana na wizara ya ardhi na makao, na ile amri ya kuwaondoa ma-squatter kwa alazima iyondolewe na walio athirika walipwe ridha.

Ya kumi na moja, ni kwamba sheria ya uridhi wa ardhi ya marehemu iondolewe kortini na irudishwe kwa kamati za vijiji, yakiendeshwa na ukoo wa jamii hio.

Ya kumi na mbili, ni wale wote ambao walihusika na land clashes watambuliwe na washtakiwe, na ile reporti ya Akiumi kuhusu vita vya kikabila, ichapishwe, na wale walio udhirika na vita hivi vya uchomaji wa nyumba zao na unyakuzi wa mashamba yao, walipwe ridha.

Ya kumi na tatu ni kwamba, kuwe na siku maalum ya maombi ya watu walioadhirika na vita hivi, na wahusika wasameheane, na waliochochea wastakiwe na kufungwa kwa kitendo hiki cha kinyama, “national cleansing day”.

Ya kumi nane ni kwamba, wale ambao wamefanikiwa ki-elimu, na kupata kazi, wasipate mashamba ya bure, badala yake wapewe nafasi kununua ploti mjini.

Ya kumi na tano ni kwamba, kesi za mashamba zifanywe na wazee wa vijiji au ziwasilishwe kwa tribunal court.

Ya kumi na sita ni kwamba, majina ya watu wale wamepewa mashamba iigizwe kwa computer ili kuzuia unyakuzi wa mashamba.

Ya kumi na saba ni kwamba, squatters wanapendekeza serikali ya majimbo, tuwe na majimbo matatu. Tuwe na bunge, na kila bunge liwe na mbunge wa kuwawakilisha na tuwe na urban councillors.

Ya kumi na nane ni kwamba mwananchi akishikwa azuiliwe kwa muda usiyopungua masaa mtano.

Ya kumi na tisa, vyama vya taifa viwe vitatu pekee katika nchi nzima.

Na ya mwisho ni kwamba kura ya chief na councillors ifanywe kwa mlolongo. Nafikiria hayo ndio maoni yetu.

Com. Dr. Monik Korir: Asante, umependekeza kwamba kuwe na majimbo matatu, moja unaweza kututajia ni yapi?

Simon Twere: Majimbo hayo matatu yawe za yuni yaani Western, na Kirinyaga, na Pwani.

Com. Dr. Monik Korir: Na umefikiria mipaka?

Simon Twere: Sijafikira mpaka, lakini kitu ambayo kimefanya tufikirie hivi ni kwamba kuna watu wanatoka mbali wakija upande huu, na wanchukua mashamba na wanatufukuza nje ya mashamba. Kwa hivyo masquatters wamekuwa na namba kubwa sana katika Transzoia kutokana na wale wantoka sehemu zingine.

Com. Mosonik Korir: Okay, na vyama vitatu tu vya siasa ni vipi?

Simon Twere: Hapo sitaweza kufafanua lakini italingana na vile wananchi wenyewe wanawezachagua ni vyama gani vinaweza kuanzishwa viwe vyama viatu.

Com. Mosonik Korir: Asante sana, tumesikiza nafikiri ni Onesmus Muchiri.

Onesmus Gichiri: Asante sana, kwa majina ni Onesmus Gichiri na nina mapendekezo machache hapa, kama ifuatavyo. kwanza nasema tuwe na serikali moja ya taifa.

Uchaguzi wa Rais: Rais achaguliwe kwa asilimia hamsini na moja ya kura zote ambazo zinapigwa na awe na umri kwanzia miaka thelathini na tano kwenda juu. Atumike katika vipindi viwili vya miaka mitano, mitano. Awe mlinzi mkuu wa Katiba ya nchi, na anaweza kuachishwa kazi yake ikiwa atavunja Katiba ya nchi na kuthibitishwa na bunge ama mahakama.

Mawaziri: Rais achague waziri mkuu, ama mawaziri wa serikali yake, na ni lazima kwanza wathibitishwe na bunge ya kuwa ni watu safi wanaofaa kwa hizo kazi.

Utawala: Wakuu wa mkoa, na wakuu wa wilaya, na wa tarafa, wateuliwe na serikali lakini ma-chief na machief wadogo wawe wanachaguliwa na wananchi wenyewe ili ndio tuwe na utawala bora.

Bunge: Bunge la nchi liwe huru kwa mambo yake bila kuwa chini ya mamlaka yoyote nje ya bunge, ispokuwa wanachi walio wachagua na vyama vyao. Jambo lolote ambalo linaleta tatizo likubaliwe kupigiwa kura na wananchi ili liamuliwe.

Sehemu ya uchaguzi: Kila sehemu ya uchaguzi itengwe kulingana na watu, sio eneo, ili kuwe na uwakilishi sawasawa. Mbunge kwa mfano akiwa anachaguliwa na watu hamsini elfu, sehemu zote ziwe na watu hamsini elfu ambao watawakilishwa na mbunge moja, ili waweze kutumikia raia sawasawa.

Tume ya uchaguzi: Tume ya uchaguzi iwe tume huru baada ya kuteuliwa na Rais na kukubaliwa na bunge iwe inajisimamia yenyewe ikiwa na mamlaka yake yenyewe ili kuweza kumaliza ulaghai wa uchaguzi, na itakuwa na kwenyekiti wake, ambaye atasimamia hio tume kwa miaka kumi na tano.

Mahakama: Mahakama ya nchi iwe huru ya kazi zake. Jaji mkuu atateuliwa na Rais na kukubaliwa na bunge na hapo atakuwa na jukumu la kuteuwa majaji wenzake, na ambao atawatoa majina yao kwa Rais wa nchi, naye rais atatoa hayo majina kwa bunge, na yakishahitishwa, watafanya kazi hio yao. Jaji mkuu anaweza kuondolewa tuu ikithibitishwa na bunge, ana anaufisadi, ama kezi yake haiendelee vizuri.

Ulinzi wa nchi: Rais wa nchi ndiye amri jeshi mkuu, kuteua wakuu wake wajeshi na kadhalika. Mbali polisi wa nchi ninapendekeza wasimamiwe na mkuu wa polisi ambaye awe huru kushika, kushtaki bila upendeleo, na awe ameteuliwa na rais na kuthibitishwa na bunge, na anaweza kuondolewa tuu ikiwa itathibitishwa ana makosa na bunge ama mahakama, na atumike kwa muda wa miaka kumi na mitano.

Uhuru wa watu. Ninapendekeza ya kwamba, hakuna mtu, iwe hakuna mtu ambaye anshikwa na kufungiwa zaidi ya masaa ishirini na manne kabla hajafikishwa kortini.

Uchaguzi na ushindi wa chama: Chama kikiwa kimeshinda, na hakina wingi wa wabunge wa kuweza kuunda serikali, kiko huru kuungana na vyama vingine kuunda serikali, na pia kila chama kilichojipatia 5% ya kura zote zilizopigwa, kitambuliwe kama chama halali, na zilizochini ya asilmia tano, zisiandikishwe ama zitutwe.

Ardhi: Katika ardhi ninapendekeza tuwe katika nchi yetu ya Kenya na kiwango cha mtu kuwa na ardhi kwa sababu kuna watu wengi ambao wana ardhi.

Ikiwa mtu moja awe na ardhi, pengine awe na kiasi cha akari hamsini, katika ardhi ambao ilikuwa na wakoloni. Lakini ikiwa ya nini ardhi ya jadi anaweza kuwa na kiwango chochote, manake, ile ni ardhi ya jadi, na sehemu zile zingine ambazo zinabai zingawiwe maskini. Asante sana hio ndio maoni yangu.

Com. Mosonik Korir: Okay, kabla ujaendoka, nitakuuliza, ulisema Rais awe umri wa miaka thelahini na tano kwenda juu, na juu kuna kiwango chochote ama hakuna?

Onesmus Gichiri: Juu hakuna kiwango chochote kwa sababu yeye yaani anatumika vipindi viwili tuu vya miaka mitano mitano (laughter).

Com. Mosonik Korir: Asante sana, okay Johnstone Boit.

Jonstone Boit: Asante sana Dr. Mosonik Commissioner. Jina langu ni Johnstone Boit. Maoni yangu ya kwanza, ningependa kusema ya kwanza election ya mayors, chairmen ya county council iwe directly. Pia kipindi ya miaka miwili ambaye iko kwa Katiba ya saa hizi, iongezwe iwe miaka tano. What I mean baada ya kuchaguliwa imalize miaka mitano. Isiwe miaka mbili, baada ya miaka miwili wachaguliwe tena. Pia councillors ambao wanaochaguliwa wawe na kiwango cha elimu, hata kama hawatakuwa na kiwango cha elimu ya juu sana lakini at least awe na masomo ni mtu ambaye anaelewa lugha ya Kingereza, Kiswahili, ni mtu ambaye anajua kwandika hizo lugha zote mbili, kwa ma councillor.

Wajumbe pia wawe na kiwango cha masomo, sababu Katiba ya saa hizi inasema mbunge anapotakiwa awe mjumbe anafanyiwa language test. Kwa hivyo hio language test mtu yoyote tuu anaweza kuelewa Kingereza, anaweza kuelewa Kiswahili, na hata hakwenda shuleni, kwa hivyo hta wajumbe wawe na kiwango cha elimu.

Mambo ya parliamentary seating: Iwe ni kama kazi yoyote, kazi ya kawaida. Isiwe tu safari tatu kwa wiki ianze Jumatatu mpaka Ijumaa, kwa sababu wakati huu, pengine Jumanne mpaka Alhamisi, na pia mjumbe akikosa kuhudhira kikao, asilipwe, sababu kuna wambunge tuu, mbunge naingia kwa bunge anaandkisha jina yake na kutoka nje. Kwa hivyo nasema, mbunge asipohudhuria kazi yake, asipata mshahara. Pia speaker awe na uwezo ya kuweza hata kufukuza huo mbunge akuje kwa raia ambaye alichagua yeye, tulize ni kwa nini hachukulii kazi yake maanani. Kusudi kusema hivyo, Katiba ya sasa inasema quaram ni wajumbe thelathini. Kwa wakati huu tuko na wajumbe mia mbili ishirini na mawili, lakini tunashangaa sana tunaposikia kulikwako, walikosa quaram ya wajumbe thelathini. Wale wengine karibu mia moja themanini walienda wapi? Kwa hivyo ninaweza nasema wajube hawachukulii kazi yao maanani.

Pia napenda kusema ma-councillor, mshahara yao iwe ikitoka central government sababu kuna municipality zingine hawana pesa, and that is why mara nyingi unaona ma-councillors hawana pesa. Kwa hivyo ma-councillors wangelipwa kutoka serikali kuu yetu. Kuna maona watu wengine walisema ya kwamba, mjumbe asipofanya kazi yake vizuri ama councillor, aitwe nyumbani ili tunaweza kuachisha yeye kazi, na tuchague mwingine. Maoni yangu nasema, naona hio sio kama kawaida sababu, kawaida wakati mjumbe anapochaguliwa ako na mpinzani wake. Nikipita kwa mfano wale walikuwa wapinzani wangu ndio watakuwa wa kwanza kuniita nyumbani, halafu warudishe ule mwingine. Kwa hivyo hio ni kumanisha tutakuwa na by-election every week ama kwa kila siku. kwa hivyo hio nasema tu akikosa, tupatie nafasi ya miaka mitano amalize kazi yake, akifanya vibaya basi baada ya miaka mitano, hatuwezi kuchagua.

Pia maoni yangu, kuna wale watu ambao walistaafu, pia hao watu waangaliwe sana. Sababu baada ya mtu kustaafu hakuna mtu anajali. Kuna wale ministry walikuwa wakifanya kazi, pengine anaongezwa pesa, pia ningepomba ya kwamba, yule mtu ali-retire kama bado ako hai, hat ayeye pia aongezwe pesa, na maslahi ya hawa watu ma-retiree yaanagliwe.

Mambo ya kilimo pia iangaliwe sana, sababu hio ndio uchumi ya mwananchi, the common man. Kwa hivyo mambo ya kilimo iangaliwe. Mambo kama loan, yapatiwe wakulima ili mkulima awe na nguvu zaidi.

Pia mambo ya masomo: Masomo iwe free education kwanza, tuseme kuanzia nursery mpaka secondari, sababu kuna umaskini mingi na watu wengi hawasomi sababu ya ukosefu wa pesa.

Pia security ya mwananchi iwe ni lazima. Watu walindwe, kila mwananchi awe na hio uhuru ya security.

Pia mambo ya health: Health tuseme kwa wakati huu sasa pengine wagonjwa wanaweza enda hospitalini na hakuna dawa. Kwa hivyo hio ni kumaanisha watu pengine hawangaliwi kwa upande wa health, kwa health, kwa hivyo mambo ya hospitali, district hospitals, hata sehemu ya vijijini zipatiwe dawa.

Pia uchaguzi wa urais: Maoni yangu itakuwa ya kama mwenzangu, iwe na vipindi viwili vya miaka mitano mitano.

Pia tunataka serikali ya the government of national unity, serikali ya watu wote, na pia katika hio serikali iwe na prime minister, awe na two deputy prime minister, awe na vice president.

Ya pili ni land issue. Wakati wa kupeana mashamba pia ma-squatter waangaliwe zaidi, wale hawana mashamba. Ya mwisho kuna maoni ambaye wajumbe wanasema wakati huu. Wanasema wanataka kuongeza muda wa bunge, na maoni yangu naona isiyongezwe muda wa bunge hata siku moja. Contract yetu na wajumbe ni miaka mitano. Pia hio mishahara mingi ambayo wajumbe wanajiongezea, pia tunasema hapana. Hizo pesa ni mingi na tutafanya nchi iwe maskini. Kwa hivyo hio extension of parliament, tunasema hapana.

Pia ya mwisho kabisa, commissioner wenu ambayeni Professor Yash Pal Ghai, yeye alihakikishia wakenyans kwamba, yeye atafanya kazi yake, mwisho wa mwaka huatamaliza Katiba. Kwa hivyo mimi na challenge yeye ya kwamba, if he is a real professor amalize kazi yake kabla mwisho wa mwaka huu, and thus I think hio ni message lazima ajue hio, asante.

Com. Mosonik Korir: Okay, asante sana, ningetaka kuuliza tu kiwango cha masomo ya mjumbe, hakutaja.

Johnstone Korir: Awe tu na masomo kuanzia tuseme level ya 'D' level kwenda mbele, diploma mpaka degree.

Com. Mosonik Korir: Joseph Maritim.

Joseph Maritim: Kwa majina ni Joseph Maritim. Maoni yangu ni kuhusu maneno ya mashamba. Vile mimi najua, mashamba, yaani ilikuwa kwa mikono ya wakoloni. Yametangazwa mzuri, labda iliwekwa kwa magazeti, na wenye walikuwa na uwezo walinunua na pesa zao. kwa hivyo kwa maoni hata ule mtu ako na acre elfu kumi, hio ni mali yake iheshimiwe. Mtu, sioni maana yakusema ipunguzwe shamba, mtu kutoka acre hamsini mpaka kumi, sababu hio kitu iliuzwa, ilitangazwa.

La kufauta hio ni nguvu ya wambunge, wambune sisi ndio tuliandika hawa, waliomba sisi kazi, na kila mara tunashangaa wakijiongezea pesa mpaka nusu million, bila kuuliza sisi tajiri na tuliandika hawa. Hio inatumiza, sababu hio ni taxes yetu, na hali watu wengine wameumia kuna walimu wameenda college, wameenda wapi, wajapata pesa, na tunasikia mshahara hakuna. ya wajumbe hii inatoka wapi?

Uwezo ya Rais ikuwe kwa wananchi. Tunashangazwa saa zingine watu kule mbungeni, wabunge wanapigakura ya kusema hatuna imani na Rais, na mbunge huyo ni mfanyi kazi kama rais. Tulichagua hawa wote, hawakuchagua Rais, wananchi walichagua rais. Kwa hivyo, wawachie wananchi kazi yao, kama Rais amekuwa mbaya, amalize yake tuje tufute yeye wakati ya election, sio wambunge wanafuta rais huko bungeni, na yey ni mfanyi kazi kama yule yule, kwa hivyo kwa hayo machache ni na malizia hapo.

Com. Mosonik Korir: Asante sana. Atanasia Siayo.

Atanasia Siayo: Mimi ni Atanasia Siayo, na mimi ni kundi la squatter alliance Transzoia. hawa watu wanaitwa squatters, ni watu walikuwa na makao yao, na ninashindwa ni kwa nini wanaitwa squatters ni elfu kumi, hawa watu ni squatters elfu kumi, na hawa ndio huchagua wambunge kwenda parliament. Kwa hivyo ninashindwa sana wakati tunasikia squatter alliance ni watu elfu kumu. Wambunge ambao twachagua wanenda kufanya nini huko kuhusu hawa watu? Ndio pendekezo letu unaona mambo kama hayo serikali ichunguze sna kwa maana kuita mtu nchi yey tajiri, na wote ni sawa na wale watu ambao wako elfu ishirini ambao wanaitwa squatters. jambo hilo tunaona kama lichunguzwe.

Tena mamlaka ya Rais. Kwa maana Rais maana anachaguliwa huko maneno na yeye ni mwananchi kama sisi tu, hata wakati atarudi nyumbani atakuwa kama sisi. Tunaona yeye anaweka sisi mzigo kubwa sana, wakati sisi tunachagua mjumbe, yeye anakwenda simamisha mbungi huyo, na kazi inianza kufanyika na wambunge wengine wa pande zingine, hilo jambo tunakataa, inaumiza sisi sana kwa maana sisi wenyewe ndio tuliweza kujua makosa yamjumbe wetu, na tupe Rais maoni ya kusema umlete wengine mwingine akuje wafanye kazi hapa.

Jambo lingine kama maoni. Sisi tushaumia hapa Transzoia sana, wakati tuliletewa hapa DC akitaka kusaidia sisi mambo yetu, tunastuka anashatolewa bila sis kuelewa nini mbaya. Kwa hivyo jambo hili sisi wote serikali itusaidie kama mambo kama hayo.

Jambo la pili maoni ya watoto. Watoto wapewe uhuru sana kaw maana tuna watoto na watoto hao wamekwisha umia na serikali iko, na tunashindwa ni serikali gani ambaye tunafuata.

Jambo lingine ni maoni ya mwisho, sisi tuko na shida sana hapa Transzoia, na shida hii inaletwa na wale watu wanaitwa matajiri. Sikui kwa nini wanaitwa matajiri, ndio wananyakua vitu huko, ndio wanaitwa matajiri, na sisi tunaitwa maskini, tunataka hili jambo serikali ichunguze sana, na kuhusu mambo ya mbunge, kuhudimu vipindi viwili, tunaunga mkono ikuwe hivyo. Rais tena ikuwe hivyo, na mambo ya majaji ichaguliwe na wnanchi, na mambo ya bunge kuhairishwa, wabunge wapige kura ipitishwe, sio Rais kusema tuu ninahairisha bunge kwa mambo ya kutokea tu. Mambo ya sehemu ya uwakilish kama hapa Transzoia ma-home guard waondolewa, kwa mana hawa wameshaleta shida kwa serikali, kwa maana wanauwa watu. Halafu mambo ikifika namna hio wanarudisha mambo kwa serikali, serikali ndio inasema tuuwe. Mambo ya serikali kutembea na bunduki ipigwe marufuku. Askari kutembea na bunduki imeshajaribu kuleta matope kwa serikali, iondolewe, kwa maana hata unaweza pata home guard anateembea na bunduki na anasema anatumwa, na kumbe hatawengine naona hawa usiku na bunduki ati naenda kungoja. Mtu fulani. Hio maneno unaona serikali itusaidie kuondoa hawa watu wanaitwa home-guard, tujue serikali ma polisi peke yake, yangu ni hayo tuu.

Com. Mosonik Korir: Asante, lakini umesema nini kuhusu hawa ma-squatter wapewe, elfu kumi. Umesema walikuw na ardi yao?

Atanasia Siayo: Nasema walikuwa na ardhi mahali walikuwa wanaishi, kwa maana a\wakati mzungu aliingia humu, alipata hawa watu pale, na watu wameshatolewa na watu wanajiita matajiri wakiweka hawanje kusudi wawafanyie kazi kwa mashamba yale walimiliki ya wazungu kwa mambo ya ujanja yao.

Com. Mosonik Korir: Okay asante.

Atanasia Siayo: Asante.

Com. Mosonik Korir: Stephen Anguli.

Stephen Angulu: Kwa majina najulikana kama Stephen Were Angulu, ingwaje waliotangulia wameongea mingi ambao nilikuwa nayo, nitayarudia mengine kwa haraka tu, lakini ningependa appointment, important kwa serikali kama judicially, kwa parliament, ikuwe ratified na parliament yaani president naweza chagua cheif justice, anaweza chagua hata even ministers, lakini wakuwe ratified na bunge letu. Tena katika Katiba yetu tungependa impeachment clause iweze hkuwekwa katika Katiba. Yaani president ama mfanyi kazi yoyote wa serikali anaweza kuondolewa, na hata kushtakiwa akiwa anafanya makosa, kwa sababu wakat huu tunaona ni kama wengine wako juu ya sheria.

Jambo lingine ni kuhusu mahahakama. Ningependekeza kuwa na supreme court ambaye itakuwa na judges wasaba na ambao wathudumu kwa maisha, na wanweza ondolewa na bunge ama commission, ambaye inaweza kaa na kujadili labda jaji amefanya kosa.

Upande wa mashamba: Kuna wau matajiri sana anaweza kuwa na shamba hata acre elfu kumi, na atu wengine hawana chochote. Ningependa serikali iweke ceiling kiwango fualni. Mtu hawezi kumiliki ardhi kupita kiwango fulni especially white highlands ambazo zilikuwa za wazungu.

Kura ya president: presidentail elections ningependekeza zifanyike miezi mitatu bada ya kura ya parliamentary na civil, kwa sababu hizi kura zikiwa congested zote kwa wakati moja znaleta confusion kwa sisi wapiga kura.

Jambo la mwisho ni kuhusu wambunge wetu: Tunajua wambunge ni sisi tunawachagua waende kutuwakilisha na sioni vile mfanyi kazi ama mtumwa anaweza kuwa na powers zaidi kuliko yule anayemtuma. Wanafika kule wanjilindikiza mishahara za juu, wanabadilisha Katiba inakuwa viraka viraka inakuwa kama kitu cha kuchezeza. Ningependekeza area fulani fulani za katiba zisiweze kubadilishwe na wambunge hata kidogo, ni warudishe kwetu. sasa hivi wanjadili juu ya kutengeneza sehemu zingine tisaini za uchaguzi za constituencies. Hio ni very important matter yenye inatakikana ananchi wote wahusishwe. Sio wale wangangane tu kule wakijua tuta-enefit kwa zile 90, wanajua yenyewe. They can split even kenya into a million constituencies tukiwachia ile uhuru, kwa hivyo wawe na uhuru kidogo. Asante.

Com. Mosonik Korir: Nikikuuliza kabla ujaondoka, ukasema kuwe na ceiling ya ardhi in the white highlands. Lakini hukusema kiwango hicho kiwe kipi?

Stephen Angulu: Ningepedekeza ceiling iwe acre thelathini na minimum iwe mbili.

Com. Mosonik Korir: Simon Rotich.

Simon Rotich: Kwa majina ni Simon Rotich niko hapa kama msemaji wa kibanasi na niko na maoni ningeweza kutoa katika kikao hiki ya commissioners kwa siku ya leo.

Ya kwanza ningependa kuguzia umiliki wa shamba. tumeona katika nchi yetu ya Kenya tukufu, tatizo kubwa imekuwa katika upande wa shamba, na upande moja mimi nimesha onelea ya kwamba ingerekebishwa ni upande wa, kama kuna mzozo upande wa shamba tuseme umiliki, isiwe mtu binafsi lakini iwe community. Kwa sababu tuseme hivi ni kwamba, kama kuna tatizo wakati mwingine tumeona kama sehemu za mipaka ama mtu ameuziwa shamba na wakati mwingine akalaghai mwenye amemuzia. Ingewezekana ya kwamba wazee wa sehemu ho wahusishwe isiwe mahakama. Tumeona tatizo kubwa mtu mwenye

kulaghai shamba anaenda kufnaya mambo yake kule na ma-advocates na wale wenye wako huko mahakamani pale, unaltewa tu karatasi, shamba uliuzwa hata jamii hajui, unakuja unatupwa nje na hio ni maoni na matatizo. usuluhisho wa shamba urudi kwa community isiwe mahakama, asante.

Ya pili ningependa kugusia mambo ya maneno ya jamii. Katika nchi yetu ya Kenya tumeona mambo ya familia imezoroteka, kwa sababu ya mabadiliko ya namna tunavyoweza kuishi katika dunia hii wa sasa. Mabadiliko hatuwezi kuepuka, lakini tunakubaliana. Ningependa kusema ya kwamba tunatatizo ya watoto na yatima. Hawa watoto mayatimu ni wetu, na lakini tumewakataa. Namna tinaweza kuwatunza hawa tumesema tutaendelea maisha yao tukiomba pesa ya msaada ili tuwaendeshe, hapa mimi nimeona hatuwezekani na si mzuri. Nchi yetu ingeonelea ya kwamba hawa mayatima itengewe fedha fulani katika V.A.T. ya kuweza kuwalinda hawa watoto na kuwaendeleza. kwa sababu niseme hivyo hawa watoto ni wetu, sio wa barabarani, wazazi ni sisi, wazazi ni wale wanafanya kazi wakatwe hizo mshahara zao iende katika hazina ya haw watoto mayatima.

Upande mwingine ningependa kugusia kwa upande wa jamii kama wakati huu sasa wakati wa virusi vya ukimwi, kama moja either afariki katika boma pengine baba afariki, na huyu mama pengine amewachwa bado na umri wa chini. Pengine kuna madama drum zingine wanasema tumridhi, hio isikuwe lazima. hio inakuwa kwa hiari, kama kuna utamaduni zingine ama jamii zingine zinakubaliana na maneno ya uridhi, lakini mama mwenyewe uamuzi ni wake. Isiwe jamii yetu inafanyanga hivi, aridhiwe sio lazima.

Upande mwingine ningependa gusia ni upande wa serikali, ni upande wa parlimanet. parliament ikatwe itoke mbili. Niseme hivyo ni kama vile hata juzi wabunge walijiongeza mushahara mikubwa mikubwa bila concern wananchi waliopeleka watu kule. Tuwe na mbunge ya wakilishi na ya senate, na hio ya senate hii itakuwa inafanya kazi moja kwa moja na mkasa. katika nchi yetu anayefanya kazi kubwa ni mzee wa mtaa, lakini atambuliwi, na hata mshahara apewe. Ie kingekuwa kiziri wakati huu parliament itokee mara mbili huyu mkasa atafanya kazi na mjumbe moja wao wa hawa anawakilisha bunge zetu mbili. Ndio huyu anajua mwananchi kawaida anajua kila jamii, sio kama vile sasa mjumbe wetu sasa hawezi jua kule jijini kuna tatizo gani, anasikia tu kwa wanasiasa wenzake wengine, nambapo maneno inaweza pelekwa kisiasa. Lakini kama mkasa watakuwa wakiwasilina moja kwa moja na mjumbe, hakika maneno ya mwananchi itasikwa kulw mbele, na itawakilishwa vizuri.

Upande mwingine ningependa kugusia ni upande wa uongozi: Kama kuna mtu anaweza kujitokeza kama anataka kugombea kiti chochote, pengine ya udiwani, pengine ya ubunge, pengine ya ucheif, mambo yake isiangaliwe. pengine kama yeye ni mtu duni. Lakini tunataka tu yule mtu quality builder, pengine ana elimu na huo anastahili. Sio tu kusema tu ooh boma ya wenye wanajiweza, wenye wana mali, lakini mradi tu anweza kuongoza, ana akili timamu, na ana elimu ya kutosha, na anaewza kuongeza.

Basi upande mwingine ningependa kugusia tena ni upande wa cultural issue: Mwafrika hawezi kutenganishwa nautamaduni

wake. Ingawa tunasema tumebadilika lakini wengine bado wanendelea nazo, na iwapo kama kuna jamii ambao wangepende waendeleo na utamaduni wao Katiba iwatambue. Isiwanyanyase na ku-brand hao. Majina ya bai bali kwa sababu niseme hivyo, katika sehemu yetu wakati mwingine pengine kuna utamaduni fulani tuseme kama jamii yetu. Kuna wale watakaofanya kimila mwezi wa nane, kam Wabukusu, na December Wanadni. Katiba itambue hawa pengine kama shule ifungwe. iwe tu inasemekana kama kuna DC, anaweza leta mgongano katika administration, provincial administration wakati shule inasemekana inafungwa tarehe fulani. Jamii wenye yewe wameanza kufunga shule tayari wanaenda kupeleka watoto kimila. Hio ina utaratibu fulani ambayo sheria inatambua hawakufika siku fulani, wanashughuli fulani, na ambapo haitaeleta mkorogano kati ya serikali na huyu mwananchi.

Basi ningependa tena kugusia upande w elimu: Elimu tumeona imekuwa ni gharama, na ingewezekana elimu iwe ya bure, kwanza darasa ya shule ya msingi hadi ya upili, na ningependa kugusia tu jambo moja ambapo iwapo kama mafunzo itatolewa, lakini iwe katika kiwango fulani ya kusema tuseme pande ya family planning. Tatizo imetokea kwa watoto wengi waendi shule ni umaskini imechangia, na tena jamii yetu imepanuka. Imeleta ama tumezaa watoto wengi na yenye hailingani na raslimali. Ingekuwa na kiwango ya kusema elimu itapeanwa katikakila jamii kwa watoto fulani, na ukipitishwa hapo utalipa tax. Hio kama nielinganisha na kama vile tumekuwa na raslimali ya shamba, usipoweza kustawisha yote, ile ingine unakuwa taxed yenye ujustawisha. Ningependa kusema kulinganisha na hio ya kwamba, kama unaweza kuwa na watoto kumi katika jamii yako, familia kwa mfano, na unataka serikali ikufunzie wote, ule naye akuwe naye wengi, hio nayo haitaeleta, na hatutaweza. Ingewezekana kwamba watot kiasi fulani serikali ikushugulikie, kiasi fulani kama utapisha itakuwa ni jukumu lako tax utakuwa unalipa. Ingawa mwendo au shughuli itakuwa ni moja. Lakini utagaramia sehemu kubwa kuliko tuseme tunaachia serikali jukumu yote na ile hali sisi ndio tunachangia.

Fridah Juma: Mutaweka sheria kwa maana, hatuna electricity na hakuna mahali ingine nitapata kuni. Mna-burn, ku-burn, so hiyo mti nimepanda lazima nikate, nipasue, nipikie. Msipotusaidia, tutakuwa tukienda kwa jela watu wengi sana. Kwa maana serikali haikunipandia hiyo miti, ni mimi mwenyewe. Shamba nimenunua mwenyewe, si unaona vile waafrika wanapeleka wengine, wanatunyanyasa! Hiyo ni kunyanyasa na wanakupeleka huko, unalipa pesa na hiyo ni corruption ndio tunastop. Thank you.

Com. Dr. Mosinik arap Korir: Na mama kitu cha mwisho ni kwamba fursa hii tumewapata raia wananchi wa Kenya, kusema kuhusu Katiba na kujaribu sisi wenyewe kurekebisha Katiba. Lakini Katiba ya kwanza ile tulisema asubuhi, ya independent constitution, iliandikwa na wakalishi wa vyama vya siasa, politicians. Halafu wamebadilisha Katiba karibu mara arobaini, sixty-five percent, bungeni. Hii ni nafasi tu, hii ya kwanza kwa raia wa kawaida kusema kuhusu Katiba, lakini kusema ukweli, wabunge wako na wanaweza kufanya hii kazi bila sisi.

Na wanaweza kubadilisha hata kwa siku moja, unajua sheria mingi wamefanya hivyo, kitu kama hicho.

Fridah Juma: Kwa hivyo hyo ya trees mutapeleka parliament?

Com. Dr. Mosinik arap Korir: Yeah.

Fridah Juma: Thankyou very much!

Com. Dr. Mosinik arap Korir: Now kila mtu ambaye atakuja, ahsante sana, ufanye tu mapendekezo na tafadhali tusirudie

yale ambayo mtu mwingine amesema tayari. Ama ukirudia usema, ninakubaliana na wale wamesema kwamba ardhi iwe namna hii, halafu tumalize. Hii list ni ya watu wengi, na tutaketi hapa mpaka tumalize. Tafadhali sasa Shadrak Muthai, hayuko sahi, Kikemboi Matonye.

Kipkemboi Matonye: Bwana commissioner, mimi nataka kuongea sana kuhusu, ooh, jina yangu ni Kipkemboi Matonye na ninataka kuongea kuhusu serikali, vile serikali ningependa iundwe.

Mimi ningependa serikali iundwe ya majimbo. Kwa hivyo serikali hii sas tuko naye nimeona ina viongozi wa kwanza walifanya, vile walifanya ni, walisema eti kila mtu aishi mahali anataka kuishi lakini kuona viongozi hawa, ni viongozi ambao aliona kabila yao ni wengi ndio wakaanza kusema hivyo. Hawakujali makabila zingine wadogo wadogo. Sana sana ningependelea serikali ya majimbo, na hiyo jimbo ipatiwe uwezo ya kuamua vile wanataka kuongozwa.

Mimi ningependelea kutoa maoni kidogo kuhusu tuseme kama sasa tukiona towns, municipality za Rift-Valley, tukianza Laikipa, unaweza kuona ya kwamba kabila zingine wamekuja wamechukuwa hata u-mayor hiyo town na wenyeji wako wapi? Kukuja tena Nakuru, wamevamia hivyo hivyo na mpaka sasa hata wako katika mashambani. Na kufikia Eldoret, Eldoret sasa ukiona mac-councillors ya huhko ni karibu nusu ya wale wenyeji na nusu ya wale wengine wanatoka nje. Lakini sasa hivi karibuni hiyo town itanyakuliwa, na makabila zingine nahata sisi, tuseme wenyeji wa hiyo town ama wenyeji wa Rift-Valley, tunasiki auchungu sana. Tunaenda kupotea pole pole, pole pole. Hata hapa Kitale yenyewe, sasa ukienda hapo ni For-Kenya, tuseme na hawa tena ni makabila zingine zinatoka nje ndio wanakuja kuchukua hizo mitaa.

Na vilevile Kapenguria hapo, vile waenyeji wa hapo waluhuzunika sana mpaka hata wakatimuwa wengine. Sasa, tunaona ni kheri Katiba ibadilishwe ili maafa zingine hazitatokea katika sehemu zingine za nchi. Hii tunataka hivi, mama wew ni mwenyeji wa hapa upatiwe haki, kama wewe ni mwenyeji wa hiyo jimbo upatiwe haki ya kuongoza, upatiwe haki ya kupiga kura, upatiwe haki ya kukata kura lakini kama wewe umetoka nje usipatiwe hiyo uwezo ya kufanya hivyo. Ila maovu isitokeleze tena, ndio unaona sana katika vita za clashes sana zilitokea, zilitokea kwa sababu makabila zingine zimetoka kutoka nchi zingine, wamekuja wamejaa na kuharibu kitamaduni ya makabila wengine. Ndio tunaona ni kheri hao watu kutoka nje wasipatiwe haki ya kupiga kura katika hiyo jimbo, nakupatiwa haki ya kukata kura katika hiyo jimbo, lakini waenda mpaka jimbo yao, waende wafanye hivyo. Ili maafa yasitokezee tena, kwa vile ukisikia hat akutoka central hakuna vita ilitokezea.

Com. Dr. Mosinik arap Korir: Lakini uendele, umemaliza hapo, endelea sema ingine.

Kipkemboi Matonye: Basi, kwanzia tena kuhusu sehemu za land. Yaani vile wanasema eti kila mtu ako na uhuru ya kuenda kuishi na kununua shamba katika sehemu yoyote katika Kenya. Ninasema hiyo ni tena kunyanyasa makabila wengine wadogo. Ninataka uende ununue shamba katika hiyo sehemu na unapitia ma-council ya elders katika hiyo mashamba. Ningependelea hivyo, mtu asiende tu hivi hivi na kuenda kununua shamba na kukaa, wale mila yake sio wanashikana na yule na wana-cause

vita.

Haya, kuhusu elections: Sana sana, Katiba vile wanawake wanasema eti tunataka uchuguzi, waatiwe thirty-percent, mimi ninaonelea hiyo sio haki kwa sababu wanaweza weak viongozi ambaye wananchi hawataki. Ndio mimi nataka, ningependelea hivi, wanawake wajitokeze kwa wingi, wafanye campaign na lakini si eti kupatiwa tu hivyo hivyo. Sasa Mr Commissioner nafikiri nimemaliza zangu

Com. Dr. Mosoni arap Korir: Ngoja kidogo! Bwana Kipkemboi, wewe umesema unataka serikali ya majimbo, lakini kuongea kwako inaonekana serikali yako inataka iwe ya kikabila. Vile kila kikabilia iko, hiyo ndiyo serikali ungetaka? Sawa, hiyo ni swali moja na tena swali la pili wewe ni Matonye. Una haki kweli unajua ni nani mwenyeji wa sehemu Fulani ukifuata historia? Unaweza ukajua, kama vile tunajua wale ambao huyu ni historia ya mkubwa sana, anajua watu wengine pengine walitika Partia, wakateremka wakaingia Zaire, wakakuja Sudan, ndio maybe wako pande hii. Sasa tufuate wenyeji hadi wakati gani? Ndio tukaweza kujua wenyeji ni Fulani, tunataka utusaidie kama Tume.

Kipkemboi Matonye: Vile tutajua wenyeji ni tutajua wenyeji vile uhuru ulivyotokezea, vile kuanzia uhuru na kuanzia.

Com. Dr. Mosoni arap Korir: Please, haya ni maoni yake, tuyasikize ukiwa na, excuse me, unajua, tusikizane, maoni anatoa tunasikiza lakini kitu cha muhimu una haki ya kutoa yako. Tafadhali tusipige kelele. Jibu, ukiuwa unajibu. Kwa sababu kwa mfano, uangalie mahali kama sasa Transzoia na mahali zingine mahali makabila yamechanganyika kwa uwingi. Ningetaka kujua utaji wake ni akina nani walikuwa wenyeji wa kwanza. Kwa sababu kama unasema ni Fulani, vile vile tunataka tujue ni muda gani nyuma, kwa mfano, ukifuata historia ya watu wengi kama Wamaasai, Wamaasai wanaweza wakasema Nairobi ni yao yote, si ni hivyo? Wakamba wako karibu hapo, wanaweza sema sehemu Fulani ya Nairobi ni sehemu yao. Infact wanasemanga Jomo Kenyatta ni yao, lakini sasa tunauliza je sisi kama wanakenya, kitu moja ni umoja tunataka ya wanakenya, na vile vile tunataka tujue ni nyuma vipi tutajua wenyeji.

Na wewe umesema baada ya uhuru, si ni hivyo? Basi hiyo ni maoni yako, asante! (laughter).

Asante Mr. Kipkemboi Matonye, Leonard Nyongesa please, Leonard Nyongesa, Isaac Wafubwa, Isaac Wafubwa? James Ligaraba, Huyo ni Isaac Wafubwa, ni wewe uharakisha tafadhali mapendekezo, mapendekezo...

Isaac Wafubwa: Mimi ni Bwana Isaac Wafubwa na nitapendekeza kidogo. Mimi ni mkaaji wa trans Nzoia, nilizaliwa Trans Nzoia, nilipozaliwa Transzoia na nikalelewa hapa na pengine serikali haijanikumbuka kuhusu vile mimi ninaishi. Sina kipande chochote cha shamba na nina mtoto ambaye anahitaji uridhi wangu. Je huyu mtoto ninapomlea kwa njia ya shida, na anaendelea kukua na mimi ninaendelea kukua mzee na sijamfanyia chochote, sina mahali pa kuweza kumtafutia.

Siku za nyuma, ataniulizaje, hilo ni pendekezo langu? Serikali ingetafuta jukumu la kuweza kuwatafutia walio wanyonge wapatiwe kijisehemu ili tujiendeleze, tuwe na matumaini ya kuweza kuwaonyesha watoto wetu wa nyuma ya kuwa huu ni uridhi wangu ambao nilupokea na serikali ilinipa.

Na vile mimi naona ya kuwa mama hawezi kukuzaa na akose kukunyonyesha, si utakufa? Utakufa. Nchi na serikali ndio mama yetu, ambayo ataweza kutunyonyesha ili tukuwe. Lingine; ningesema hivi kuhusu police. Nitasema police haina utamu katika nchi yetu. Sheria ingepitishwa hivi, polisi yyote akitoka katika stesheni, awe na warrant na hii warrant ifuatwe tu ikimfukuza mwenye mshukiwa nayehitajika. Utakuta huyu polisi anapopewa hiyo warrant ya kuweza ku-arest huyo, anasakanya hii vijiji yote. Anasakanya hii vijiji yote, kuenda kufika kule, alipitia hapa sasa hapa kazi imekwisha, sasa ataenda hivi. Akirudi kwa station, ana nyama ya mama amenunua. Amejiita ni mwanaume mwenye uwezo kwa nyumba yake, na gorogoro nyumbani kwangu imechukuliwa. Watoto wangu wamelala njaa. Kuhusu polisi hilo ndilo kosa. Na hilo nino ndio sana serikali inasema raia hawasikizani na polisi. Ni kutokana na neno kama hilo, ndio imeleta uadui katikati ya raia na polisi. Tunataka sheria ichunguze hilo neno.

Com. Dr. Mosoni arap Korir. Pendekezo kwa hivyo?

Isaac Wafubwa: Sheria iandikwe kuchungwa pale, mimi nikiwa na kosa huyu polisi atoke kwa station, aje na warrant na anaimbie Bwana Isaac Wafubwa, unaitwa katika station, unakosa hili na hili na hili. Na atoke pale moja kwa moja, akirudi kule, asikoroge vijiji. (laughter) kwa maana hawa wengine sio wa hiyo kosa, ni mimi ndio niliyekosa, Isaac Wafubwa.

Com. Dr. Mosoni arap Korir.: Asante.

Isaac Wafubwa: Nitasema tena kuhusu sisi ni wazazi, sisi tuna watoto vijana na wasichana. Utaweza kukuta, kijana wa mtu anajaribu kudanganya mtoto yako msichana, unasema nitakuo na sina mwengine ila ni wewe tu! Baada ya kufika mwisho, amempa mimba. Mwishowe wanendelea akicheka, barabarani anasema bwana huyu nilimpiga booty bwana. Sasa huyo nimesongesha kando, sasa nataka kale ka-Catherine ka Fulani.

Nitapendekeza, kitu cha kwanza sheria ingepitisha hivi, si amempa mimba, kitu cha kwanza huyu kijana ashtakiwe kwa kuambukiza huyu msichana ukimwi. Kitu cha pili, amempa mimba.

Com. Dr. Mosoni arap Korir. Yes please, umalize tafadhali, haraka haraka, please.

Isaac Wafubwa: Nafikiri, hata ingawa vijana muko kwa barabara hiyo munasema mimi ni, munanikosea, lakini sio mbaya sana. Rekebisha huo mtindo na tuelewana wewe unapotafuta mchumba, umtafute kwa njia zako zote na ukiamini ya kuwa ni huyu tu mpaka siku ya kiyama. Usiwe na mabadiliko, penekezo si nimetoa?

Kwanza, utashtakiwa umempa ukimwi, ya pili umempa mimba. Hiyo ndio upendekezo.

Com. Dr. Mosoni arap Korir.: Asante sana, haya James Ligaraba.

James Ligaraba: bwana mwenyekiti wa commissioner ya siku ya leo na wasikilizaji wengine, mimi jina langu ni James Ligaraba. Mimi ninataka maoni yangu;

Oni yangu ya kwanza ni kuhusu office ya president. Ofisi ya president ina mamlaka mengi sana, ambayo ilipewa na Katiba kuna kwamba ofisi ya president vile ilipewa na Katiba, inasemekana kwamba rais hawezi kushtakiwa mahakama. Na hii imefanya sasa rais amepewa mamlaka ambayo anaweza kutumia vibaya. Kwa hivyo napendekeza ya kwamba, katika Katiba ambayo tunarekebisha au kuunda, rais apelekwe mahakamani.

Pendekezo langu lingine, ni kuhusu provincial administration. Provincial administration kutoka katika office of the president tunaona kama haina kazi ambayo inatufaa nayo. Kwa hivyo katika Katiba ambayo tunairekebisha, mimi ningeonelea ya kwamba tufutilie mbali provincial administration. Kwa sababu katika provincial administration, kuanzia chini kabisa, tuna ile mtu anaiwa mugaa. Unatoka kwa Mugasa na team yake, unakuja kwa sub-chief, sub-chef na mamlaka yake hii yote mnajua. Inaenda namna hio, namna hio kwa chief, kwa D.O., D.C., P.C., na kadhalika, kwa hivyo kuanzia kwa D.O., unakuta kwamba the D.O. ana departments of the government ana ofisi ya..

Com. Dr. Mosoni arap Korir:Lakini nikuulize, si upendekeze tu, ufutilie mbali yote, wachia hapo tu.

James Ligaraba: Pendekezo langu lingine ni kwamba, katika chapter two section thirtheen, tunaelezwa ya kwamba kuna allowance nyingi ambazo rais anapewa baada ya kustaafu.

Hizi allowances mimi naona ni nyingi sana, na hasa kwa rais bada baada ya kustaafu. Na tuko na rais mwingine ambaye ako kwa kiti. Zile allowances nataka zikatwe, kwa sababu inaonekana inaonkana kama tutakuwa tunalopa rais wawili mishahara, na hatuna resources za kutosha.

Pendekezo langu lengine, kuhitimu kwa rais. Katika nchi hii tuna wasomi wengi na ninapendekeza ya kwamba katika Katiba chapter two section two; inatakikana iongezwe ya kwamba, rais wa nchi hii awe msomi wa cheo cha chini sana ama amehitimu darasa, kidato cha nne. Kwa sababu atakuwa anaongoza pia wale watu wengine ni wasomi.

Pendekezo langu lingine, ni kuhusu mamlaka ya ministers na ministries. Katika nchi hii tunalia umaskini na kumbe kura pesa zingine ambazo tunatumia ambazo hatungekuwa tukitumia. Unakuta katika wizara kuna minister, kuna ma-assitant ministers

wawili au watatu, na katika kila ofisi ya assistant minister kuna ma P.S. na kadhalika. Hii yote, kazi inaweza tu kufanywa na minister mmoja, na ikiwezekana awe, na assistant mmoja. Natu-save pesa mingi ambazo tunalipa duplications of offices.

Na nikirudi kwa ile provincial administration, mahali nimesema hizi ministries unakuta kila section ina full office, hizi ministries zingekuwa zingerudi chini ya, kamani ministry of education iwe tu kwa minister wa education. Isipatikane tena section kwa D.O., kwa D.C, hapana, iwe tu kutoka juu na inakuwa delt with the ministry of education. Na kadhalika, na kadhalika. Nafikiri kwa ufupi hayo ndiyo mapendekezo yangu.

Com. Dr. Mosoni arap Korir: Asante sana. Mary Chang'wong?

Mary Chang'wang: Commissionre na wanachi wenzangu ambao tuko pamoja, kwa majina ninaitwa Mary Chang'wang. Yangu ni machache tu, sina mengi ya kusema na unajuwa pengine tungetakea mueleke jinsi ya kuongea na mahala nitakosea, mtanisaidia. Mahali mnaona nimeenda nje ya point mtanirudisha, museme kwa sababu sitaki kupoteza wakati hapa.

Ya kwanza ni kwamba, nafikiri katika nchi yetu ya Kenya mimi naona sisi wananchi wengi hatuko aware of sheria yetu ambayo jinsi inatokuwa kutuchunga ama jinsi inatakiwa kutusaidia katika nchi yetu. Na pengine watu wengi wangukuwa hapa lakini kwa sababu hawaji hata pengine hiyo sheria tunatakiwa tufanye nini ama tukuje tuongee nini ndio imetufanya hata pengine hatungeweza kukuja hapa na kusema nini, ikwa hivyo sijui hii sheria itafanyw namna gani, ili kila moja awe aware of juu ya maisha yake ama sheria ambaye inatakiwa kumsaidia katika nchi yake.

Nafikiri sijui tunaitaje watu wakusomesha. Kwa sababu kuna watu wako assigned ile ya nyumbani, pengine hata hawajui maana na uzuri ya kitu kama hiki. Na pengine angekuwa na maoni mazuri ambaye angeweza kuja kutowa.

Ya pili nilikuwa nataka kuongea mambo juu ya uchanguzi. Inasemekana vile tumekuwa tukisikia ya kwamba pengine kwa mtu kwenda kama councilor ama kwenda kuwa mbunge ama nini, lazima awe na masom fulani. Na kuna watu wengine Mungu amewaumba naturally wanaweza kuwa viongozi. Ndio ni mzuri akuwa na masomo, lakini ukona wasomi wengi pengine wenya wako na standard ya juu hata pengine hatachukuwa wewe pengine jinsi, yule mwengine hata pengine hajaenda shule, hajasoma. Sasa hii sijui kuchaguliwa pengine unataka kukuwa councilor ama nini, sijui kama ni maoni yangu kwamba itatengemea vile awatu wampenda. Pengine akuwe mtu pengine ni social, pengine ni mtu atasikia shida yangu na pengine awe ni kongozi mzuri pengine amepewa hiyo talanta na Mungu. Lakini tukisema tunataka kuchaguwa pengine mtu ya standard ya juu zaidi, pengine ameenda mpaka university ndio akuwe kiongozi, pengine atakuja kutukoroga zaidi. Sasa sijui tutaona namna gani, pengine mtu ako hapa karibu. Ama tuseme in a village, ama in alocaiton ama in an area mzim. Pengine hatuna mtu amesoma kiwango ile mnataka hiyo. Sijui itakuwa namna gani ili tuweze kuchaguwa mwenye anaenda kuturepresent huko mbele.

Kwa sababu uongozi unatoka kwa Mungu, kwa hivyo hiyo sheria lazima iangaliwe vile wasaidia watu.

Ningependa kuongea juu ya mambo ya mashamba. Sisi watu wengi tuko so much innocent, procedure ya kununua mashamba katika nchi hii, you find now unakuja kununua shamba kutoka kwa mtu. Tunafanya vitu kienyeji kiasi ya kwamba hatujui sheria yetu. Unanunua shamba kutoka kwa mtu baada ya kununua shamba mnafanya pengine kienyeji. I don't know how niite kienyeji, sijui nitaitoan tu vile tutaisikizana na mtu kwa sababu namjuwa ni yeye. Kidogo pengine baada ya muda kwa sababu ya corruption na nini, kuna mjuwaji anajuwa mahali ya lands pengine mahali wataenda kitu wataenda kufanya kwa lands nini, pengine mtu amekupendua tayari! Unashtukia ndio hao umechukuliwa high-court, umeenda kushtakiwa katika high-court.

Pendekezo langu ni kwamba, tunataka kufunzwa hii mtu mdogo huyo mwenye ako innocent hajui hata sheria ni nini, hajui hata shamba ukinunua unatakiwa ufanye nini. Tufundishwe tujwe ukinunua shamba kwa mtu unatakiwa ufanye namna gani na ningependekeza ya kwamba hasa sana tuanzia nyumbani, tuchukuwe village elders wapate kujua, watu wa raia wapate kujua, wakisha kubaliana na kwamba hiyo shamba hauwei kusikizana na mwenzako mununue hiyo shamba. Na kama kuna shida yoyote, watu wa karibu hapo ndio waweze kufanya hiyo kesi. Kenye inanisumbua ni kwamba, kwa nini mtu unakuta umepelekwa high-court, haki surely hujui kitu yenye unaenda kusema unapata uole advocate yako. Sijui kazi hii ya advocate, unasikia ni watu wenye wanatusumbua, they are corrupt lakini si ni serikali wanataka ikuwe namna hiyo. Unaingia huko ni kazi yako ni kufuata hata hautajuwa kitu yenye anaenda kusema. Kazi yako ni kufuata, ni maisha ama umenunua ukiwa huko. Hata hajui maneno ya shamba hii vile ulinunua. Lakini sasa anafanya ni camera. Tutasaidiwaje ili hii kitu irudi nyumbani wenye wako hapa karibu wapate kujuwa hii sheria. Kwa sababu inatumiza sana unaenda huko hata unanyang'anywa kitu yako ile umetowa kwa jasho yako na haki yako ya ukweli, katika nchi hii, tunasikia uchungu sana.

Sasa mimi sijafurahia hiyo kitu. Ninataka sheria ya ku-cover sisi. Kuna wazee sijui wenye wako kwa chief wamepewa watusaidie hiyo kazi. Mara unaenda kuskuma unaambiwa hawa nao wanasukuma pande hii, huku umeshikwa advocate, judge ako anakusomea, hajui wewe hajui huyu hajui ukweli kama ukweli umeishi hiyo kwa muda hiyo yote na inaweza kutupwa. Kwa hivyo tunataka kama tume mtusaidie jinsi hii kitu irudi kama ni maoni yangu, irudi mpaka nyumbani, though we are all corrupt now, hata wetu wa nyumbani hata ya mlango kwa hata mtu ya mlango anaweza kukuta akisema pengine hakujui lakini practically ama ukweli kama umekuwa ukikaa na watu mzuri watakujuwa na watakusaidia.

Kwa hivyo muangalie masheria ya \shamba,. Kwa sababu saa zingine tunaenda land board. Mimi nikafikiria siku ingine kumbe nimeenda land board pengine hiyo kazi imesiha ifound myself niko kwa high court. Kwa hivyo serikali watusaidie sana kwa hasa kwa upande wa manenoya mashamba kwa upande huo.

Ingingine, kama nimeongea nje ama ndani mutanisaidia na mutanisaidia mahali point inaweza ingia. Point ingine ni kwamba, sasa katika sheria ya sasa, sijui kama ni sheria ama nimekuwa nikisikia. Kwasababu mimi nimetoka nyumbani uko reserve kabisa, ni kwamba tumeolewa na katika sheria ama nimekuwa nikisakia kidogo mara nyingi watu wanasumbuka kwa ajili ya bwana akifa. Pengine kwa mfano, akitangulia kufa na wazee wa siku hizi sana sana wameenda wanachukuwa wamama wawili ama nini yaani imekuwa ni shida ya kwamba, sijui shetani ameingia watu kuna shida nyingi. Sasa mzee akikufa unaambiwa lete mali ya certificate ndio uonekane ni bibi yake. Jameni mama mzee mwenye amekwisha ana watoto na wameowa na kila kitu na siku hiyo sio kupewa mali ya certificate, tutasaidiwaje katika nchi yetu? Nitatupwa nje nikilia bababarani na ni mzee wangu? Na pengine ameleta ile ndogo ndogo akuje kwa hii na pengine hata amebadilisha hiyo title deed. Halafu mimi nitaenda, amepatia huyo I mean marriage certificate. Mimi sijapewa marriage certificate, sisi wamamam tutasaidiwa naman gani?

Si ni lazima kila mtui awe na marriage certificate, kuna akina ngoko hawana marriage certificate sasa, sijui hiyo sheria itatendenezwa namna ani, ili wengine wasiweze kumia. Kwa sababu nyakati yenye tuko wazee wako mbio sana, wanaowa mbili mbili na tunatupwa kabisa. Kwa hivyo mutusaidie hapo.

Ingingine kuna kitu nilikuwa ninataka kuongea juu yake, sijui kama inaletwa mbele ya tume ama nitaongea out of the point. Nilikuwa nataka kuongea juu ay watoto, kuna kitu inanigusa juu ya watoto wa shule. Watoto wa shule munaona wakati hii vile wanendelea, kuna shida ya mambo ya madawa ya kulevyo. Na watu wanaharibu hata watoto wetu wanapeleka hata mambo ya madawa ya kulevyo kwa mashule. Sijui watachukuwa sheria gani? Munaona inaendelea kuwa even worse. Watoto wanajuwa wanafanya nini, sijui ni sheria gani wanaweza tumnia ili tusaide watoto wetu wahepe na vitu kama hivyo.

Na ingine nilikuwa nataka kusema hivi, watoto wetu wako shule. Mimi ni mzazi, wewe ni mzazi, ndio tutarajia atleast kuna mtoto mmoja anakuwa mbaya. After school mtoto wangu ataonekana yeye ndio senior ya kulead wengine wasome shule. Akitoka shele, ataandikwa recommendation kwa shule ya kwamba huyu mtoto ni mbaya. Huyu mtoto atakuja outside na amekuja na hiyo recommendation. Surely alikuwa mbaya shuleni na ni mwananchi anakuja Kenya. Hamutofunga yeye aende nchi ingine. Ameandiwa recommenation mbaya, how do you expect my child aandikwe kazi na ako nao bad recommendation? Si atakuwa muuwaji zaidi hata atauwa president, kwa hivyo muangalie mtasaidiaje mtu kama huyo.

Com. Dr. Mosonik: Sasa si umalize

Arap Korir:

Mary Chang'wang: Ninamaliza. Nafikiri ingine ni kwamba sijui nimesahau point ingine. Nafikiri wacha, nafikiri ni juu ya wacha tu nimalize, nafikiri nimesahau, ahsante, sitaki kupoteza wakati. Thank you.

Com. Dr. Mosonik: Mama mwingine ni Angela Adonyi. Tuharakishe tafadhari dakika moja, mbili

Arap Korir:

Agela Adonye: Mwenye kiti watenda kazi, wasikilizaji na wasalimu wote. Majina yangu naitwa Angela Adonyi. Ninapendekeza kutowa maoni kuhusu wafungwa na zaidi ordinary remands.

Ordinary remands, si vizuri mtu yaani wapeleke udanganyifu kwa station polisi kwamba mtu amefanya hivi na kumbe hajafanya. Na polisi anamukamata, rimandi muda mrefu, judge anaitisha hawaendi, kupelekwa kotini kwa judge tena ni shida akae tu kwa simiti, chawa zinamuuma maji hakuna ya kuoga chakula kidogo na baadaye anawachiliwa anarudi nyumbani. Hakuna afya, kwa hivyo naomba serikali iweze kusaidia watu kama hao. Atakuwa amewacha watoto wake nyumbani, hawana usaidizi watkauwa tu wanaiba vitu vya watu ndiposa wakule. Boma imevunjika, hata mimi mmoja wao saa hizi sijui watoto walitawanyika tu na kuandikwa kwa watu kutuchungia ng'ombe. Kwa yale ambao hakuwa ya kweli.

Com. Dr. Mosonik: Asante na pole kwa hiyo mambo asante umemaliza?

Angela Adonyi: Na sana naomba serikali isaidie sisi wamama. Mzee anakudanganya tu wewe kwenyu, anakuoa, kufika huko anakuwacha watoto, chakula, shule, mavazi kila kitu. Hakuna wewe umeshindwa, unaenda kuowa tena mweingine anakuwacha kwa boma (laughter from audience). Ndio huyo anatoroka anakuwacha kwa boma sasa watoto wengi wameshindwa hata mama ameshindwa kupeleka watoto shule kusema kwa jili ya kushindwa na masaidizi yoyote.

Com. Dr. Maranga: Mama ungetaka wazee wafanyiwe namna gani ndio wachukuwe mzigo wako? Ungetaka tuweke sheria kuhakikisha wazee wanaoangalia watoto wao?

Angela Adonyi: Wazee watosheke na kile ambacho alichu nacho, ni hayo tu. (laughter from audience)

Com. Dr. Mosonik: Ahsante sana, Leah Kimani?

Arap Korir:

Leah Kimani: Ahsante sana commissioners, mimi ninamachache tu yakuongeza yale wenzangu wamepitisha. Ni kwasababu, ninakushukuru kwasababu umeona ya kwamba wamama hawakuja wengi maana wameambiwa wakae huko nyumbani kama unavyosikia. Wanalazimishwa kukaa. Kwanza mimi ningeomba, ningependekeza ya kwamba, jina langu ninaitwa Leah Kimani. Ninataka kupendekeza ya kamba kuwe na civic education, ili watu waweze kuelimishwa waweze kujuwa wajibu wao na waweze kujuwa wanatakiwa kusema nini na kufany nini, kwa wakati gani na katika hali gani, watu wakisha elewa mambo hayo, mambo yatakuwa rahisi kwa kila mtu ndipo unaona ya kwamba watu wakija hapa wamechanganyikiwa. Hawajui kama ni kutoa maoni ama ni kuleta malalamishi yao ya nyumbani. Kwa hivyo serikali ifanye mpango wa kuelimisha watu kama jinsi mnavyoenda na mambo yatakuwa rahisi kwa watu.

Jambo la pili, ningependa ya kwamba, wanawake kwasababu mara nyingi hawawezi kushindana na wanaume, katika kupiga kura, hawana pesa za kumkimbia hapa na pale, ili kuweza kusimama katika ubunge, ningeomba ya kwamba serikali ifanye kama vile nchi zingine zinafanya kama Uganda waweke sehemu moja ya tatu, kuwa ya wanawake. Na katika kila wilaya, ikiwa wilaya ina constituency kama tatu, constituency moja waachiwe akina mama. Na hiyo iwe katika rotation, isiwe kamam

ni chereangani, miaka mitano hii ni mama miaka mitano mingine ni mama, hapana iwe rotated yaani ikiwa chereangani leo mama miaka mitanok, Sabot mama miaka mitano miingine , iwe rotaion namna hiyo. Na wakati inakuja nomination, wale nominated members, wamama wapewe two-thirds. Kwa sababu hawa hawana mbinu za kupigania sana. Wapewe two-thirds na hizo two-thirds kila mkowa upewe mama mmoja.

Utaweza kupata wakati mweingine nomiation inafanya, na inapewa mkowa mmoja, nomination zote, kwa hivyo mikowa miingine ukiangalia hata sasa haina waakilishi. Kwa hivyo two-thirds ya wale kumi na wawili iwe ni wa mama hiyoitakuwa kama wamama wanane, na kila mkowa upatiwe mama mmoja. Na ikifanywa hivyo itakuwa ni vizuri.

Na tatu ni kwamba, wafanyi kazi wote, nataka kupendekeza ya kwamba wafanyi kazi wote wamapoajiriwa kazini waandike ni nani atakuwa mridhi. Kwa sababu mambo haya yameleta shida sana, hasa wakati mzee anatangulia ndio amekuwa akifanya kazi, na mama yuko pale, mzee anapotangulia anakwenda, mama akitaka kuenda kufatilia mambo hayo inakuwa ni shinda sana. Lakini ikiwa mfany kazi atajiandikisha kama mzee ya kwamba ikiwa mimi nikiondoka yule mtu anatakiwa kupewa marupurupu yangu, ni mke wangu na jina lake ni hili, na watoto wangu na majina yao ni haya, basi mzee akiondoka na mama akienda itakuwa ni rahisi kupata mambo hnayo. Ama the other way round, mama akiwa anafanya kazi naye atajiandikisha ya kwamba nikiondoka, mzee wangu ndio atapata faida zangu na mzee wangu ndio huyu na watoto ndio hawa.

Kwa sababu hii imewachukuwa wamama wengine hata mpaka kukufa bila kupata fiada hizo. Haya ndiyo mapendekezoyangu maana yale mengine ninayo, watu wamekwisha ya toa kwa hivyo ninawashukuru sana na mubarike. Ahsante.

Com. Dr. Mosonik: Ahsante, na councilor Musa Kosgi wa Kaplamo yuko? Maurice nafikiri Wanyonyi? John Bosire, Rotich John Kirwa?

Rotich John Kirwa: Bwana chairman, commissioners na watu wa CKRC wote na raia ambao wamekuja kutoa maoni yao. Mimi naitwa Rotich. Ningependa kutoa maoni yangu kwa commission hii.

Jambo la kwanza, ambaye ningependa kusema ni CKRC ni commission kubwa nchi hii. Na mpaka saa hii haijaandikwa kwa Katiba. Sijui security yenyu ni nini hapa. Ningependekeza ya kwamba, commission ambaye imejikilika nchi hii iwe na security of ten year wakati wako kwa kazi na wafanye kazi yao vizuri. Kwa sababu bila hiyo hatuwezi kujua mambo ya kesho itakuwa nini,. Na hatutaki kesho tusikie commission ya Katiba hakuna. Tunataka iweko mpaka wakati wa election ikishwe, mpaka mwisho ya kumaliza kazi yenu sawasawa, tupate Katiba mpya ambayo itakuwa nuru ya nchi hii. Hiyo ni jambo la kwanza.

You need recognition and you need to be in the books. Jambo la pili, ni jambo ambalo tunaelekea kuenda, mambo elections, conduct of elctions; elections ya macouncillors, ya majumbe, hata ya presidents, mimi nimewai kusimama kutafuta kura ya ubunge mara mbili na yale maneno niliyaona na ile vituko niliyaona ni mengi, na ningependekez ya kwamba wakati election inakuja tunataka a level playing field. Tunatak uwanja ambao iko wazi kabisa. Ambaye kila mtu ambaye anatafuta kura atafute kwa haki na kwa kweli na apigiwe kura kwa haki na kwa ukweli.

Mambo ya kuzima toa usiku, ama kufukuza watu kwa campaign, ama kuuza watu wengine hiyo itolewe kabisa kabisa, na kitu ambayo inaweza towa hiyo ni sheria kali kwa election officials. We must have control, we must have proper regulations to regulate conduct of elections. And then the most important part of it, the implementation has to be thorough. It has to be transparent, it has to be accountable. Mambo ya zamani ya kupata watu wakienda mlolongo, laini mfupi ndio inachaguliwa, kuenda bunge laini mrefu ndio inapotea. Hiyo tukomeshe hiyo. Hiyo ndio ufisadi ambayo tunapigania tupoteze. Ufisadi ukiingia kwa kura, hata haki ya raia inapotea na mtu amekaa kwa laini the whole day, alafu amechaguwa mtu anajuwa amechanguwa na ni wengi, mwishowe hayuko, hii ni mbaya.

Baada ya hiyo, kama una malalamishi baada ya elections, unatakiwa kuenda high-court, ukienda high-court na kesi yako sheria ya high court na sheria ya eletion petition lazima ifwatwe, moja kwa moja kwa sababu kama mtu, if somebody is a crimed and he has an injustice to fight he has to be given a chance to fight thoroughly and to the finality by election, the people of chereangani did not disqualify me. I was disqualified elsewhere. Dispite a clearance certificate in my pocket. So some of these

things are wrong and we cannot have them in a multi party era like now. Elections petition are supposed to be a heard as quickly as possible because the complaint is immediate and should be an immediate remedy to it.

Mtu akifanya petition na ikakaa miaka tatu, ama miaka tano, mwishowe ashinde hiyo petition, where is justice here? Justice iko wapi? Mtu amekaa nyumbani miaka tano na alikuwa ameshinda, hakiya raia iko wapi? Kwa hivyo ningependekezaya kwamba kama petition iko, ifanye within six months, haki ya raia irudi kwa raia raia wenyewe waamuwe safari ya pili. Ndio kweli itaonekana na haki ya mpiga kura atapata.

Jambo la tatu, ni kuhusu local authority, local authority ni serikali ile ya nyumbani. Yangu ningependekeza ya kwamba we have a devolution of power from the central government, to the local authority. Tunataka serikali ya nyumbani hapa iwe na nguvu kuliko juu, ili raia awe na haki ya kusikizwa, ningependekeza ya kwamba councilor ambaye anachanguliwa, awe ni councilor, awe ni chief, awe ni mtawala kamili. Na baada ya hiyo, mjumbe ambaye anapewa cheo kwa constituency, awe mjumbe ambaye anafanya kazi zote za serikali. Kwasababu ana mandate ya raia afanye kazi zote, kwa hivyo hiyo local government ipewe nguvu kuliko wakati huu ili iweze kulete services kwa raia.

Chairman ya county council, kama Nzoia County Council, tungependekeza ya kwamba awe ni mtu ambaye anachanguliwa kwa post ya chairman from every location ili awe kama DC naye awe na uwezo kama ya DC kwa sababu kama anafanya makosa na amepewa miaka mitano, tuna haki kuita yeye na kumwambia umekosa hapo, kwa sababu ni mtu ya hapa atajibu. Kama hawezi kujibu, atabadilisha mwienendo na afanye kazi vizuri. Kwa hivyo councilor afanye kazi zote kwa location, chairman ya county council afanye kazi zote kwa district, alafu central government ifanye kazi ya defence na police administration na mambo mengine.

Hiyo administration ndogo ndogo hizi zirudi nyumbani kwa sababu councilor akiwa mtu wa hapa na tukiwa na shida kwa location hii tunawea kuenda kwake asubuhi. Hawezi kuhama, atakuwa hapa tu, na kama chief ni mtu wa hapa na aliandikwa na serikali atafanya kazi za serikali, atawacha raia. Kwa hivyo anaumiza watu sana, ukifany hii unapigwa hakuna mahali unapeleka chief. Akienda huko, anasimamiwa na state council wewe napotea, kwahivyo councilor awe kila kitu kwa location. Ukitaka kumpa yeye watu wadogo wadogo, sawa. raia wenyewe watachanguwa ya kusaidia yeye kazi.

Basi mambo ya P.C. baada ya kumaliza mambo ya DO na chief na DC nafikiri PC hana kazi sasa. Hatakuwa na haja na PC kwa sababu kila location iko na mtu yake, kila constituency iko na mtu yake, na kila district iko na mtu yake, PC ni ya nini? Hakuna kazi. Basi tuwachie hapo, ya mwisho ni the executive powers of the president.

The president ni mtu ambaye anatakiwa kuheshimiwa sana anatakiwa apewe heshima. Lakini kwasababu yeye ni mwanadamu kama wengine anaweza kufanya makosa na akifanya makosa, hatuwa gani utachukuwa juu yake? Wakati huu kwa Katiba ambayo tunayo. Section twenty three, haikubaliwi mtu alalamike aende kotini kushtaki president. Hata kama mambo yamekuwa mambaya sana, huna jawabu. Kwa hivyo ningependekeza ya kwamba, the executive powers are too excessive and they should be reduced. One way of reducing the powers of the president is devolution of power from central government to local authority. Ndio uwezo uanzie ku-grasshold vikielekea juu. Kwa hivyo yangu ni kusema ile pyramid ya leadership kutoka apex kuenda kwa chini kwa base, tunataka tupenduwe base iende juu alafu apex iende chini. Hiyo misumari ya haki, ikienda chini unashika sawasawa, kwa sababu iko uzito hapo juu.

Sasa sahii haina uzito juu, upepo inaweza beba sisi, sindio? Kwa hivyo si eti powers are excessive, they should be devolved to the local authority and the few powers that are remaining should be executed with transparency and accountability and with justice and honour for the wananchi. Hayo ni yangu, so impeachment should be allowed so that those who are grieved can take legal action and be compensated for the wrongs that have been done against them. I am a victim of rigging. Supported by the executive powers. I have suffered and cherangani has suffered even today, ahsanteni.

Com. Dr. Mosonik: Okay, do we now have Alfred Keya? David Esoken? Proposals, haraka haraka tafadhali bado kuna watu wengi, tujaribu kufupisha.

David Esokon: Kwa hivyo jina langu naitwa David Esokon. Kwa hivyo wananchi wenzangu pamoja na wakuu ya Katiba, yangu ni machache ingawa ni mrefu kidogo lakini ni machache nataka kusema. Kuchanga siku ya leo kwa jili ya Katiba ya Kenya.

Langu la kwanza, nataka kuzungumza kuhusu mambo ya Katiba, tukiwa tukiskia Katiba, Kenya kuna Katiba anamalinda wananchi analinda raia lakini kwa hayo yote kwa muda ile imepita kwa miaka hiyo therathini na nane ama arobaini, tulikuwa tunakaa kama hatujui kama tuna uhuru katika Kenya yetu. Labda nataka kusema kwamba katika hii mapendekezo yangu, wenye walikuwa na uhuru katika Kenya hii ama Katiba hii ilikuwa ikilinda ya zamani, hiyo minskia kwamba ilikuwa ikitengenezwa London. Labda ni wale watu alikuwa ni watu wa hali ya juu nilikuwa ni watu wenye uwezo, kwa hivyo kwa siku hii ya leo nimeketi andike mapendekezo yetu iwe ni mapendekezo haki na iwe ni Katiba haki, uwe unatoa maoni kwetu haki. Isiwe ni Katiba tu ya kuchokoza sisi, alafu miaka zengine inakuja sisi tunabaki kwa shida, kama vile tuko naye kwa sasa.

Kwasababu kwa sasa hivi, tuna makabila arobaini na tatu katika Kenya, na hii kabila arobaini na tatu ama arobaini na mbili, wengine hata hawajulikani kama iko Kenya.

Saa hii wengine wanalala kwa barabara, hata kukufa hakuna pali ya kuzikwa, yeye anawekwa kwa barabara anawekwa kwa mtoro ya barabara. Na mimi mwanakenya ya Kenya hii.

Na wale watu wanajua mambo ya Katiba wanaendelea na kujua mambo ya Katiba. Na sisi Katiba hii, amoni yao ni kutaka kusema, maoni yangu ni kusema hivi Katiba hiyo unasema tutoe maoni, andika peleka kwa chairman iwe ni Katiba haki analinda mwananchi wa kawaida aliye yuko chini. Ingawa tuko sote sawa, tuliumbwa wote ikiwa ni mtu mmoja, ikiwa wewe ni mtajiri, ikiwa wewe ni maskini, ukiwa unalala chini, ikiwa unalala, lakini ni mtu mmoja lakini nataka iwe ni Katiba inatungalia masilahi mpaka chini, kuanzia chini mpaka juu. Isiwe juupeke yake ndio inaangaliwa na yule wa chini anasahuliwa. Kwa mfano, mimi ningetaka kusema kwa upande wa elimu, ilipoza hawa watoto masikini, Katiba inasema tupeleke watoto kwa shule, kule shule walimu wanataka huyu mtoto asome, hiyo shule inataka yule yuko watchman pale anataka pesa.

Na yule maskini hana chochote hana shamba, hana ng'ombe, hana chochote na huyo mtoto anatakikana aend shule. Na hiyo mzazi anakosa, namna ya kusomesha huyo mtoto. Mtoto anarudi anakuwa chokora, na mtoto anarudi sasa anakamatwa kesho, wanapelekwa cell. Haya kuna msichana wa yule mzazi maskini, amedanganywa na kijana, amezaa tayari amepata mimba na amezaa nyumbani, mama yake hana chochote, baba yake hana chochote. Kwa hivyo sasa mtoto kama huyo bado anapata taabu na hana makao, hana aina yeyote. Kwa hivyo sasa ikikuwa ni Katiba, iwe ni Katiba ya kuangalia mambo kama haya, kwasababu tunaendelea kuumia, na tunaendelea, watu wetu wanaendelea kupotea tumerudi kucheka ya kwamba hawa watu ni bure.

Pili, mambo ya shamba: mambo ya shamba ile imezungumzwa na wandugu yangu wengi, mambo ya mashamba iwe ni mahsamba haki kama shamba kama hii pahali tunakaa, kama mtu alipata kwa haki yake serikali alitowa shamba through a plan, ama ametangaza kwamba chama fulani inapea maskini. Iwe ni maskini, ile hajaandikwa kwa serikali, iwe ni maskini ule hajafanya kazi kwa serikali. Lakini unakuta mtu amechanguliwa yeye ni mbunge tumechaguwa, yeye ni P.C. yeye anakula mshahara kutoka kwa serikali na anachukua loan kutoka kwa serikali. Shamba hiyo nimetangaza kwamba fulani inapewa masikini, yeye ndiye anaenda kesho kuchukuwa hiyo shamba, acre mia mbili na tayari shamba ilikuwa ni acre mia tatu. Na hiyo wanapatia wamaskini watatu pekee yake, na anarudisha report ya kwamba shamba imegawiwa maskini.

Sasa iwe ni Katiba haki ya kuangalia masilahi ya waraia, kwa sababu tayari ni kama sisi tunadanganywa. Hata Katiba sasa vile sasa tunatoa maoni hautamini kwasababu kama ni Katiba inaweza kutusaidia, ni Katiba tunaona ama inatupapasa. Kesho mtu anachanga tie-late kwa shamba hiyo, yule maskini wa kawaida anaendelea kufanya nini? Kwisha, si ni kweli? (eeh) Kwa hivyo maoni yangu ningetaka kusema ipendekeze hivi, ningependekiza kusema kwamba mambo katika Katiba mambo ya shamba, iangaliwe sana. Na iwe ni kama ni kati kama ni shamba inapewa maskini na iwe na sheria na ubaguzi ndani, kama watu katika area hiyo kama cherang'ani watu ni mchanganyiko iandikwe watu wote wenye area hiyo, hata kama ni watu mia mbili na ihakishwe hii watu mia mbili masikini amepata hio shamba. Ndio sasa nchi tuwe na watu wote wanaweza kufaidika. Kwa sababu mtoto kama maskini akikufa, baba yake akufe, mama afe huyo mtoto amebaki pale, mtoto huyo itakuwa maisha yake

itakuwaje? Kwa hivyo lazima Katiba iwe ni Katiba haki kuangalia mambo haya.

Ya pili, ama ya tatu, mambo ya watu polisi kukamata watu. Hatukatai kama mimi nimekosa na nina haki nimekosa, kwa hivyo sheria iwe ni sheria ya kupeleka mimi kulala police, asubuhi niplelekwé kotini. Niende nijibu niandike statement yangu na ni jibu vile nilikosa. Na kama nilikosa, kule pahali nimepelekwé kwa jela, iwe jela inaenda mimi nimemaliza kifungo yangu kama nimeambiwa lima shamba nilime shamba, nimalize kifungo changu nirudi nyumbani. Ama ni ya maisha kwisha, sababu labda nimeuwa mtu, iwe ni ya kumaliza mimi ikishwe pale. Lakini naweza kamatawa na huyo mtu ana uzito, labda mwengine ameiba kitu, wakati ameiba kitu sasa fight unakuja kwa watu wote ustakiwe na ukamatwe. Mwengine huyo anasema hata huyu, tulikuwa na huyu, hata huyu nilikuwa na huyu, sasa kwasababu ya uwoga yule ameshikwa naye, wanafikiria akisema hivyo atawaachiliwa, kufika pale sasa yeye anafungwa anaka rumande karibu miezi miwili. Hakuna haki yeyote imechukuliwa na koti ya kwamba huyu mtu hana haki. Atakaa hapo miezi mbili, ndio baadaye unaambiwa sasa mambo ya, na huyo mtu amekaa nyumbani, anasomesha tayari na ameficha yake.

Kwa hivyo Katiba iwe ni Katiba haki, kuangalia masilahi kwanza wale watu wanaumia ni wale maskini watu wa chini, ndio tunaumizwa. Na wale watu wenye wana uwezo. Kwa hivyo nikimalizia, wanaingilia hii mambo ya unyakuzi. Kunyakuwa pesa, sisi masikini tunalipa kodi, mwishowe situkiona maoni kama juzi inafanyiwa budget, kuna watu hali ya chini hakuna mtu anawafikiria. Pesa inahesabiwa inawekwa kwa mfuko. Ni maana gani tuseme Kenya ni maskini na mtu ako na ndege nne, wengine iko na mandege nne, mwengine ako na acre elfu tatu ya shamba, na sisi tunaendelea na tunasema sasa Kenya yetu ni maskini. Kwa hivyo unyakuzi, kwa hivyo iwe na sheria kuangalia mambo kama haya.

Kama ni wewe ni mtajiri, upate acre hamsini imekutosha kama ni mingi zaidi iwe mia moja badala wewe uzunguke Kenya mzima kuchukuwa shamba yeyote ya dunia mzima kucukuwa shamba yeyote ya dunia mzima. Na hauta kwenda nayo mbinguni. Haya pesa ya nchi yote wewe unanyakuwa yote na kwenda nayo. Wengine wanabaki nyumbani, wanalala ni huyu kwa hivyo iwe ni Katiba ya haki na waandike repoti ya haki. Na isiwe kitu ya kubadilisha kesho, kwasababu hii Katiba yenyu ni Katiba tunabadilisha usiku na mchana. Kwa sababu hatuna hata sasa tumesema tupelekee wananchi, sasa unakuja sasa unatoa maoni, kesho maoni yetu sisi, nyinyi mnatupilia mbali. Munaandika nyingine kumaliza mambo ya uchanguzi ...

Com. Dr. Maranga: Ahsante, ngoja kidogo. Bwana Esokon, sisi kama tume ya kurekebisha Katiba, kulingana na sheria sisi tunanasa kila mtu anasema. Na wakati mwenzangu commissioner Mosonic aliwaeleza vile tutaleta report kwa constituency. Wewe kama David Esokon, unaangalia hii mimi nilisema kwa tume, hapa wameweka kambo, ndio sababu saa ingine unaona tunauliza watu maswali, munatakaje. Ndio tunataka mapendekezo ya ukweli, hatutaki mutuambie taabu zenyu bila kusema nini, mapendekezo. Kwa sababu baadaye sisi tutasoma hizi taabu zenyu, alafu kama Tume tutafanya nini? Mapendekezo. Kwa hivyo sahih hata ukitaka turudishe hiyo tape saa hii, uanze kuzungumza vile umezungumza kila kitu imenaswa. Kwa hivyo tutaandika repoti ya kweli. Ahsante. Na nyinyi mutuombe na mutusaidie.

Com. Dr. Mosonik: Okay ahsante, ninataka tuharakishe. Kila mtu ambaye akija hapa ni pendekezo dakika moja, mbili. Bado tuko wengi, reason si hata alikuja, please dakika moja mbili. Tuseme ile point tu, haijasemwa.

Wilson Siata Maika: Mimi kwa majina ni Bwana Wilson Siata Maika. Mkaaji wa hapa, mimi nitaongea juu kuhusu mamlaka ya president. President, mamlaka yake ipunguzwe kwasababu mara nyingi wewe ukisikia yeye ndiye amri ya jeshi, yeye sijui ni chancellor wa nini, na hiyo yote ni pesa ambayo anatumia, anakula pesa za serikali za bure na raia wanaumia hapa chini. Naonelea ya kwamba akiwa president a-remain tu president. Sio amri mkuu wa majeshi ama nini na kuna watu wengine ambao wamesoma kama yeye wanastahili kukaa kama yeye. Upande wa machiefs, tutasupport wenzangu chief waondolewe hata D.O. na D.C. waondolewe, wa remain tu councillor, na wabunge.

Upande wa ugawaji wa ardhi, kwa mfano area hii tuko na majirani ambao wako ni maskwota. Hao maskwota, president hatahajawahi kujali kuangalia hawa maskwota wapewe ekari fulani. Huwa unatowa watu mbali kama hata uganda, wanakuja kukaa na sheria ya Kenya hairuhusu mwana – uganda apewe shamba hapa. Hiyo kitu umetuumiza na ndio inafanya sisi, mnayoona raia wa kawaida hataki kuongea ukweli. Makabila ambayo iko hapa Kenya ni arobaini na mbili. Trans-Nzoia imebeba makabila arobainin na mbili. Unakuja kuona makabila arobaini inahudumiwa lakini kabila mbili haidhudumiwi. Hapo

tunataka sheria ya kutetea hayo makabira yote arobaini na mbili. Haswa muluhya mturukana, sisi ambao ndio sinyenge ambao tunachungia watu, kabila hizo mbili.

Na ndio unaona mawazo yangu inasemam ya kwamba kama hivyo tuwe na serikali ambao tunaita ya majimbo. Tuwe na jimbo la Mombasa kule tuwe na jimbo la central, tuwe na jimbo la mount elgon, zamani tulikuwa tunaita skumasava. Na boundary yetu ilikuwa mount longonot, kwa hivyo tupunguze hapa katikati. Hatutaweza kuvumilia na mambo mengi. Kwa hivyo la mwisho sina lingine ni hayo tu!

Com: Ahsante sana, Shadrak Mutai, Charles Opoka?

Charles Opaka: Ahsante commissioners, kwa majina ni Charles Opaka, mapendekezo yangu ni kama yafwatayo; kuhusu serikali yetu mimi ninapendekeza ya kwamba serikali ya majimbo ifutiliwe mbali. Sababu kukna sehemu zinaweza kukuwa hazina resources fulani, na zitahitaji msaada kutoka sehemu nyengine, kuhusu serikali, tuwe na serikali ya mseto. Wabunge wanapochaguliwa kutoka kwa vyama mbali mbali, tunapokuwa na mbunge wa chama fulani ambaye ana uwezo wa kutetea nchi yake na kuongoza katika idara fulani, apate kuchaguliwa.

Muda wa kiongozi wa taifa; uwe ni mara mbili ikiwa ni kipindi cha miaka mitano mitano na baada kumaliza hiyo mwengine achukuwe nafasi hiyo. Kuhusu uchaguzi, uchaguzi upatwe kufanywa wakati wa siku za kati za juma ili tusifanye kazia mara mbili ikihudumia Mungu ikiwa weekend na unahudumia uchaguzi. Utakuwa umegawanya mawazo, kama itafanya juma nne, juma tano, alhamisi, basi uchaguzi ifanywe hapo hapo kwa sababu ni jambo la kitaifa na kila mtu anahitaji ahushishe.

END OF SIDE A

SIDE B

Angalau tuwe na shule moja au mbili za kitaifa. Ili hii asili mia themanini na tano nayo wilaya zengine zipate watoto wao kuingia katika national schools, iwe pia ni universities, vio vikuu vipate kusambazwa katika sehemu mbali mbali. Ili mtoto anapolelewa central, asiwe kwa primary central, univiersity awe central. Apate kuenda mazingara mengine ili angalau hata akija kukawa kiongozi, atakuwa namna ya kutetea watu wa sehemu ile.

Tunapoteremka kuhusu discipline; hata Mungu aliweza kudiscipline Adam. Na katika mashule na manyumbani, tusipo discipline watoto jameni hata mtakuwa na zaidi na kesi nyingi na hata mahakama ishindwe kutekeleza. Kwa hivyo tungehitaji mambo ya discipline ipate kuangalia na iwekwe katika hali ya kueleweka.

Sehemu ingine ni ya mashamba; upande wa mashamba tungeweza kukuwa na mambo mawili, uende kuna maskwotas wako katika mashamba yale ya yale makubwa makubwa, wajulikane na makumbukumbu zao ziwekwe. Pia tunaweza kuwa tunawahitaji ambayo si squatters lakini uenda ikawa shamba lao ni robo acre na ni watoto ni wengi wa mitaa hata wameshindwa kujenga nyumba. Kwanini kama wakati mashamba yana hitajika kutolewa watu katika location hiyo wakuje mahali pamoja na viongozi was serikali ili ya kwamba wale wanaohitaji wapate kutambulikana mahali pale. Kwasababu mambo mengine yanafanyika huko mustuni na baadaye munakuta aliye nayo ameongezewa. Yaani ni kama wasema ni kama Bibilia inasema aliye naye aongezewe, na yule je hana, hata kiroho hawezi akapata njia ya kumshukuru Mungu?

Sehemu nyingine, tuna sasa sheria ya watoto, na tuna sheria ya kutetea akina mama, je sheria ya wazee iko wapi? Kwasababu kuna pia wamama nao wametesa wazee isipokuwa wazee hawalii na kusema kwa mfano akilia watasema sasa hii sio mwanaume. Ninatumaini kwamba ya mwisho, pendekezo la mwisho ni kuhusu imani au faith.

Tuwe na uhuru wa kuabudu Mungu wa kweli na kando wa mashetani. Hata Yesu aliweza kufukuza shetani akamwambia shetani nenda kwako. That is devil worship, thank you very much.

Com.: Mzee Obaga wacha nikuulize swali moja. Hii swala la maskwota iko kutoka Lamu, Mombasa, iko Nairobi, iko

Rift-valley. Swali ninauliza ni hili kwa wakenya, hawa maskwota ambao wanaitwa maskwota, kama serikali ikiamua leo kila mtu amepatiwa nusu acre, wamalizike unfikiri kweli tutamaliza hii problem, ya squatters. Kuna njia ingine yoyote ambao tunaweza tukawasaidia watu ambao wanaitwa maskwota. Badala ya maybe ya kuzungumuzia juu ya mashamba, kuna njia ingine tunaweza tukasaidia wakenya?

Daniel Apong: Basi ahsante sana, na sasa ahsante sana. (laughter) si wale wanakaa hapa wako na shida si mimi pekee yangu nitazungumza. Naeleza kulingana na vile tumejaa hapa mashida yetu. Naeleza D.C. na wewe kama uko hapa unisikie vile naongea. Hii ni kilio yetu kwa nyinyi wakubwa ama wewe siyo mkubwa mbele yetu? (laughter) basi usikie maoni yetu, si tunalia. Mbona hata saa hii mimi hata hakuna viatu ya rangi navaa akala. Viatu ile yakukimbiza ng'ombe (laughter). Ni kweli kabisa hata kukufa hapa ni shida kabisa. Barabara tu, kweli kabisa hata D.C. hauwezi kuona huruma kwa hii watu wanakaa wazi wazi ahsante sana. Pendekezo yangu ni hiyo mimi ni mturukana lakini nakaa area hii. Nimekuwa mzaliwa hapa kutaka kuongea hata kinandi nitasema sawa sawa hatakama (kinandi). Eeh ahsante sana, lakini Katiba iandikwe mara moja. Hii Katiba inakaa mamiaka, miaka mingi inaandikwa ndio bado. Wengine wamekuja wameacha Katikab haijaandikishwa (laughter) yangu ni hayo.

Com. Dr. Masonik: Ahsante sana mzee Daniel Apong (Laughter) John Sicharange, Edward Muluta, Joshua Wambogo, tafadhali ufupishe, tafadhali.

Joshua Wambogo: Yangu ya kwamba mimi naitwa Joshua Wambogo na kitu ile ambaye mimi nakuja kutoa hapa ya kwamba ni hii. Katika wasichana wetu wale wako manyumbani, na kijana wetu wale wako nyumbani, tunaona kama kuna shida sana kijana anashika mtoto akawa na mimba. Vile vile anataka awe na 6 na hakuna mmoja ataenda naye. Shida hiyo ikarudia wazazi. Ningetaka kusema hii mapendekeo yangu; msichana akiwa na mimba ya mtoto yule aende naye sababu hata akiishi milele na milele atapata bibi.

Ingingetaka kusema akiwa yeye anatumwa yeye, hawa wawili kwa sababu walikuwa pamoja wasomeshe huyo mtoto. Ile nyengine nataka kusem, msichana yule anajibunisha kazi ingine ya kusema (not clear) nani mimba hii anaweka wewe?

Ananyamaza, ni kama mbwa iliweka, lakini hiyo ni makosa. Aseme ni mtu sababu alizaliwa na mtu. Kwa hivyo sasa ningetka kusema yule mtoto asomeshe na watu wawili naye yule msichana asiwe akienda kutafuta mtu mwengine iwe ni pahali anakuta ya kufanya kazi. Hiyo itoke hapa.

Ile ingine, wakati tunakaa hapa tunasikia iko mali ya serikali na mimi sijui serikali iko wapi. Hata sasa mimi nazeeka sababu analeta mtu wa serikali ananiuzia mimi pahali ya bei ghali an kitambulisho mimi napata na yangu inaingizwa . ningeliza nitajua serikali ni nani? Sababu ananiuzia na muita serikali, kitabu na pewa na inapigwa muhuri, nyumaye ninahamishwa. Ningependekeza namna hii, huyu mtu anauzia mimi mali ya umma na si yake achukuliwe hatua sababu amesomeshe sheria. Hii ni mali ya umma na kwa nini anauza mali ya umma?

Pendekezo ingine ningetaka kusema katika ile watu tunachagua (not clear) sisi wenyewe tunachagua tuakasema tunawachagua hapa. Kwa hivyo mtu yoyote tukichagua hata akiwa ni nani, apewe mali ya serikali atumishe kama wale. Kwa hivyo ile ingine mimi nataka kusema hapa tuna taabu moja katika ile hata ikiwa ilirudiwa na wtu nitarudia kidogo. Ile wakili tunamweka anaweka kesi miaka mingi kama mimi najua iko pahali inamaliza miaka 10. ile nyengine nataka kusema ni hii, hiyo kesi mimi niliapa ng'ombe na mimi natambua nikiiba. Ni kwa nini mimi naekwa siku nyingi na nilitambua? Ule nyengine nilikuwa nafikiri itawekwa rumeni juu ya kufisha, sasa mimi natambua nasikia iko. Nafikiri yangu hapana endelea sana, nitawachia hapo.

Com. Dr. Masonik: Okay, ahsante mzee. Sasa tutampa kila mtu dakika moja tafadhali. Inaelekea saa kumi na mbili. Paul Omboko. Martin ama Maritim Natonyo, yuko?

Background Interjection: Nafikiri yuko

Com. Dr. Masonik: Ehh?

Background Interjection: (not clear)

Com. Dr. Masonik: Martin mwenyewe ni mwengine yule, sio wewe? Dakika moja bwana, one minute only, just make the most important point.

Maritim M: Bwana Commissioner, ahsante sana kwa kunipatia nafasi. Mapendekezo yangu, kwa vile umeniambia ni one minute ... Maritim Matonye. Muundo wa serikali mimi natoa mapendekezo yangu ya kwamba iwe federal system, iwe mambo ya majimbo.

Land issue; unajua mambo mengi, ile shida ambayo inatatiza wakenya sana ni kuhusu mambo ya mashamba. Mambo ya mashamba ndio imekuwa kama cancer katika nchi hii. Sasa mi natoa pendekezo langu, minimum iwe economical kwa kuzalisha

nchi mtu awi na 1.5 acreage na maximum I can give 500.

Secondly, kuna watu ama makabila ambaye wako chini sana haswa primitive na sehemu zao zinakuja kaliwa na watu kutoka sehemu zengine. Ile kitu ambayo ninaomba serikali ichunguze hapo kusikuweko na immigration. Waweke sehemu ambayo inatengwa kwa minajili ya indigeneous.

Na kurudi mashamba ya serikali kama ADC ambayo serikali inapatiana saa hii, ile kitu ambayo ningeonelea pendekezo langu ni kwamba mambo ya squatters imeshinda watu sana sababu karibu kila mtu ni squatter. Sasa mimi nasema indigeneous wale watu ambao wanaishi karibu na hapo, wale ambao wanatambulika tangu mzungu aende ya kwamba walikuwa wanaishi hapo, wapatiwe nafasi ya kwanza kuhusu hizo mashamba ili makabila zengine zisipotee.

Kuhusu mambo ya federal system, nimesoma ya kwamba sasa provinces imeanza kuwa ...

Com. Dr. Masonik: Umesema hiyo federal system tick ehe, sasa ni zidisho one minute is over.

Maritim M: Okay, ahsante

Com. Dr. Masonik: Thank you, Alfred Masinde Munyonge

Alfred Masinde: Ahsante commissioner (not clear). Mimi nazungumza kama mzee wa siku ziliopita. Nilikuwa nalia kwa campa na wanaandika hii Katiba

Background Interjection: Jina?

Alfred Masinde: Alfred Masinde Manyonge

Background Interjection: (not clear)

Alfred Masinde: Oh, Alfred Masinde Manyonge. Jambo langu linalo nileta mimi hapa kamishna, mimi nalia sisi wazee tumenyanyaswa. Unachukuwa watoto wa shule unawaletea video sasa inaharibu watoto hawasilizani na wazee.

Upande wa mashamba, mimi tangu mwaka wa 28 niko hapa na sijapata shamba, nilinyanyaswa na ma-settler wale waliobaki na watu wale wengine wanaitwa director. Sasa hiyo tukupeleka maneno hiyo kwa serikali inasema “kwenda tu maneneo yako mimi na kwisha sikia” na unaenda sababu hakuna pesa ya kuhonga huko.

Neon la pili, watu walifanya akili ya kusema hatutaki pombe, katika Kenya kumbe ndio wanatuletea sisi bhangi na changaa na dawa ya kulevya. Sasa sisi watu wa kula busaa tunachangaishwa (laughter). Tunaomba hiyo isaidie sisi wazee hiyo ndiyo maziwa yetu ya wazee, busaa (laughter) ni hiyo ahsante sana (laughter)

Com. Dr. Masonik: Ahsante mzee (laughter) Stephen Kiguru,

Stephen Kiguru: Ahsante sana commissioner ambaye uko pamoja nasi pamoja na staff ambao wamekuja naye. Mimi nasema sitasema yoyote. Naona saa nimefika hali ya kuelewa ni mimi kinaendelea. Yangu ni kusema nimeshukuru kwa ajili yenu, kwa kazi nzuri ambao nimefanya muda huu wote na mzidi kufikia kilele cha kuokoa wakati kwa sababu now mswahili alisema ukingoja sana matumbo yataharibika. Mimi kwa upande wangu nitatetea upande wa kanisa ya kwamba, makanisa yote yasajiliwe. Majina yangu ni Stephen Kiguru, mimi ni kutoka division hii ya Kaplamai hapa karibu tu. Kwa hivyo ni kwa sababu gani niseme juu ya kanisa, makanisa yamezidi kuongezeka hata mengine hayajulikani yalitoka wapi na mengine hata hayana mwelekeo. Ni vizuri pia hii freedom of workshop ambayo imetokea tujue inateka makanisa gani.

Kwa hivyo sina mengi nimesema tu juu ya jambo la kanisa ni kwa sababu mengi yamesemwa na kam ulivyo proposal mimi dakika moja naona imenitosha. Kwa hivyo kwa hayo machache nawaomba baraka, mtakapokuwa mkisafiri kuelekea mahali mtaend kupumezika kwa sababu wakati umekwisha mzidi kuwa nasi wakati wowote na Mungu awabariki. Kwa hayo machache Mungu azidi kuwa nanyi.

Com. Dr. Masonik: Thank you so much Stephen Kiguru. Isaac Ewei, Samwel Kariuki, Donde S. Tom, Augustino Terekon, Mkalalio Emenum, James Mutai.

James Mutai: Kwanza napend kushukuru nafasi ambayo nimepata. Wale ambao wamenitangulia jina langu naitwa James Mutai. Wengi wameongea mambo mbali mbali lakini kwa upande wangu ningependa kupendekeza ya kwamba katika tme hii ya Katiba ya kwamba ya kwanza ni mambo ya utumishi wa umma. Utumishi wa umma umekuwa na corruption mingi. Mtu anaweza kuiba ana achukuwe pesa na badala yeye kufutwa kazi na kufungwa anapatiwa transfer yaani kuonyesha aende aibe mahali anapoelekea. Kwa hivyo ningependekeza katika tume hii marekebicho ya Katiba, badala ya mtu kupewa uhamishi ni kufutwa na afungwe.

Wengi wameongea kuhusiana na mambo ya kortini na hiyo pia sitaweza kugusia kwa sababu ya wakati. Wengi pia wameweza kugusia mambo ya unyakuzi wa mashamba na maploti. Unyakuzi wa maploti ninapendekeza ya kwamba wale ambao wananyakuwa maplot na mashamba ziweze kutwaliwa na hawa ambao wananyakuwa pia waweze kugungwa.

Mambo ya nominating MPs na president, ningependekeza ya kwamba president ako na haki ya kupendekeza ujumbe lakini asipewe wadhifa yoyote ya waziri. Mambo ya majimbo, majimbo ni nzuri lakini jinsi vile wengine wanavyoelewa na kuipeleka

wanaielekeza kwa njia ingine sio nzuri. Mambo ya majimbo ninaipendekeza ya kwamba iweko na wale ambao wanaishi pale, wakaaji ambao wanaishi pale wawe na uwezo ya kusimamia rasilimali na uongozi wa area hiyo na wale ambao wanakuja kuishi pale wanahaki ya kumiliki na kustawisha mali yao pale.

Mambo ya uongozi ... sorry mambo ya agriculture, ningependeleza kama wizara ya agriculture na ustawi wa mifugo haitawaza kusimamia na kuongoza wakulima wa Kenya hiyo wizara iweze kuvunjiliwa mbali kwa sababu hakuna kitu inasaidia wananchi. Nitasema ya kwamba mwananchi amewachwa kwa sababu yeye mwenyewe anajitafutia soko, wafanyi biashara wanadai wamepewa furso ya kuagiza mbolea bila serikali kuwatetea wananchi. Kwa hivyo haina haja wizara ya kilimo ustawishaji wa mifugo kuwekwa katika serikali yetu ya Kenya. Ni hayo tu Mungu awabariki.

Com. Dr. Masonik: Ahsante, Kiprotich Mbirir.

Kiprotich Mbirir: Mimi ni Kiprotich Mbirir, yangu ingawa imemalizwa na wengine lakini nitafuatilia nitaomba msamaha mnisaidie niseme sababu nilikuwa nimepanga nikija hapa. Kwanza kuhusu majimbo, mimi naunga hiyo sababu kuna watu katika sehemu hii watu kweli ni mchanganyiko lakini ukienda sehemu zengine kama coast, kama Cnetral huwezi pata mchanganyiko aina hiyo. Kwa hivyo mimi naomba Katiba, iundwe na kama ni forest katika Rift Valley, ilindwe na wenyeji ambaye.... Na yale yatakayo tokea katika hiyo isaidie watoto wa wenyeji wa hapa. Hiyo inaisha.

Kuna sehemu ingine kama hospitali, hospitali hapo awali, serikali ilikuwa inatibu watu bure na kupea madawa lakini wakati huu wanasema ni kugawa gharama lakini unapoenda katika hospitali unaangalia ufidadi imejaa kule ambapo.

Com. Dr. Masonik: Pendekezo tutaelewa.

Kiprotich Mbirir: Mimi napendekeza hivi, Katiba iangalie masilahi ya wananchi katika matibabu kwa sababu wengi wameumia hata unaweza kufa lakini hawaangalii vizuri. Na kuna kitu moja kama ... tuna wazee wa mitaa ambayo imewekwa na serikali na wakapewa uwezo fulani ambayo sijui ni kwa nini. Mimi niliponunua shamba yangu, ilikuwa hakuna miti hata mmoja na mimi nilienda kwa forest nikanunua miti na pesa yangu na nikaja nikapanda na wakati huu ninaweza enda nikakata kukata hiyo miti, minawezaenda na panga mpaka ninarudi, ninachagua mpaka ninashindwa lakini kuna siku itazidi nitakat moja kutumia lakini utakuja ona mzee wa mitaa anazurura pale na kusema “wapi permit?” hii permit hii inasaidia nini na sijakatiwa permit wakati nilienda kununua hizo miti. Kwa hivyo Katiba iangalie hapo sana, sababu itakuja kuwa mchezo moja ambaye italetu uadui kati ya wazee wa mitaa hata mpakakwa chief. Sababu kila mtu ambaye ana akili unaelewa kabisa miti ni uhai ya mtu na lazima ukate ingine na unaendelea kupanda. Kama huwezi kuingia kwa forest ambayo imekatwa miti mpaka imekwisha na ni mali ya umma, halafu unakuja kuingilia yangu ambayo mimi mwenyewe ninaelewa? Hayo ni yangu.

Com. Dr. Masonik: Ahsante. Wesley Kandogor,

Wesley Kandagor: Ahsante, sana kwa hii nafasi. Mimi kwa majina naitwa Wesley Kandagor, mimi mkaaji wa hapa nitaenda straight kwa bunge: nigependekeza hivi, kama president anaenda kwa vipindi viwili, miaka 10 hata mbunge aende vipindi viwili.

Na hivi vipindi viwili, miaka 5 inakuwa ni ya kuchunguza monitoring. Tutakuwa na commission katika kila constituency ambayo inachunguza vile anafanya kazi. Ikiwa atafanya makosa, sasa atakuwa recalled baada ya wakati wa pension, kwa sababu nimesikia kuna pension huwa wanapewa, hata pewa kwa sababu amefanya makosa.

La pili, naenda pia kwa mishahara ya wabunge: wasiwe wao wenyewe wanapitisha mishahara yao. Tuwe na commission katika kila constituency ambaye wanachunguza kwa sababu kama mbunge huwa anafanya harambee kwa area yake anafanya kazi mzuri, then wacha report itoke pale kwamba huyu mtu anahudumia watu vizuri. Wasiwe wanaketi kwa dakika moja na wanapitisha pesa na kuna wengine huwa wanlia wanapewa mishahara ya chini sana. Kwa hivyo tuwe na commission katika kila constituency ambayo wanatoa pendekezo kwa mishahara ya wabunge, sio wao wenyewe.

La tatu ni kwamba candidate ama wenye anataka kugombea kiti cha ubunge, councillor ama rias asiwe anaambiwa resign because that is a shed technique. Huyu mtu apewe resign na agombee hiki kiti. Akikosa, sasa tutakuwa tumepoteza utu na alikuwa na maoni mazuri ama alikuwa na maendeleo kuhudumia watu wake. Kwa hivyo huyu mtu apewe ruhusa.

La nne; kuna pesa ambazo zinaitwa local authority transfer fund. LATF. Councillors watoe mwangaza hizi pesa ni ya wanachi na warudi locational level. We have locational development committee. Wawe wakifundisha watu “hizi ni pesa zenu na mko na kamati ya location”

Com. Dr. Maranga: I think I have 2 questions. How do you certify a degree that it is, a good degree? For example we have so many institutions now which have come up and are giving degrees. How are you going to differentiate the different degrees we are getting in this country? Like now in this country we have private universities and so on.

Saidi Morris: I would

Com. Dr. Marnaga: no, that is one question. Number two, you are saying the powers of the president remain the same. Are you also suggesting that you want the president to be above the law?

Saidi Morris: (not clear) President?

Com. Dr. Marnaga: Correct should be above the law?

Saidi Morris: I am of that opinion.

Com. Dr. Maranga: Thank you (laughter)

Com. Dr. Mosonik: And the degrees you did not tell us how to certify (laughter).

Saidi Morris: I would like those with first degrees must be from public universities not private. That be the condition. If it may be added, please do so (laughter).

Com. Dr. Mosonik: Thank you very much. Reuben Kiere, William K. tenai, na kila mtu sasa 1/2 minute, you know we are getting to 6.00 p.m.

William Tenai: Asante sana bwana commissioner pamoja na wananchi ambao wako ndni ya nyumba hii. Kwa majina yangu ni William Tenai, mimi ni mkaji wa hapa Transzoia, hapa Cherangani. Kuhusu utawala wa Rais; watu wote wamezungumzia juu ya miaka tana au miaka kumi, kwa hivyo mimi naunga hao mkono, na zaidi ya hiyo nguvu izeze kuteremka chini.

Kuhushu mapato yetu ambayo inatoka kwa ukulima wetu: Serikali imetuumiza zaidi, kwa sababu ya kutulipa malipo yetu ambayo ni mali yetu ambayo tungsaidiana kwa watoto wetu kwa shule, kwa hivyo tunachelewa. Kwa hivyo ningepomba ya kwamba, maoni yangu ningepomba ya kwamba, serikali izezi kufikiria, juu ya kulipa wakulima pesa zao, na iwekwe katika Katiba yetu. Hiyo ni sehemu ya pili.

Sehemu ya tatu ni ya kwamba; serikali wakati mwingine wakati wa uchaguzi, badala ya kutupia raia uwezo wa kuchagua mjumbe wao, serikali inaanza kusema, chagueni mtu fulani, kama kwamba wananchi hawawezi kuchagua mtu ambaye wangepombe. kwa hivyo ningepomba ya kwamba, nguvu hiyo inatokana na ule nguvu wa serikali ndio inatupa uwezo ingine ya kusema chagueni mtu fulani. Ningependekeza uwezo itoke kwa wananchi waweze kuchagua mbunge wao.

Sehemu ya nne, kwa sababu nakimbiza saa, ni sehemu ya uhuru ya kuabudu Mungu, kwa siku ambayo inawmwa hata na bibilia: Nikieleza hapo kidogo, tunaona ya kwamba, wakati mwingine tunaona kuna dhehebu ambayo inaweza kunyanyaswa ama kuimizwa, kuna kwamba, siku ambayo knisa hilo inapumzika, inalazimishwa hata na watoto, wao waende kusoma. badala ya kushiriki, maneno ya kiroho, pamoja na watoto, wao, watoto wanapelekwa shule kusoma na hiyo siki hata Mungu mwenyewe, aliweza kunakili kwa kitabu ya bibilia.

Com. Dr. Mosonik: Hiyo ni siku ya?

William Tenai: Siku ya sabato ambayo utaipata katika kitabu cha kutoka ishirini, mstari wa nane, kumbukeni hapo.

Nikienda kumaliza ni ya kwamba; kuhusu watoto ambao ni wasomi wetu, katika nchi yetu tuko na watoto wengi ambao wanasoma, lakini serikali haiwapatii kazi. Sijui tutasomesha hawa watoto na mwisho wao wawe nani, watakuwa wakora. kwa hivyo ningepomba serikali, wafikirie jambo hili. tunaposomesha watoto, tunasomesha watoto, waweze kupata kusoma.

Nikimaliza ni ya kwamba tena, uandikishaji: Ikiwepo andikishaji, hs wakati wa kuandikisha jeshi, ama plisi, wanasemekana inahitajika watoto wa foot tano, au sita, na idadi yo imesemwa pengine wataandikwa atoto arobini, sitini, hamsini. Lakini kitu ya ajabu ya kusikitisha watu, watu wanamwagoo barababarani, na kuambia, “kimbieni,mpate kufika hapa haraka”. Watakapofika hapo, wanachukuwa watu wawili, ama watano, katika district, lakini ile idadi walisema kumbe wamebeba wengine kutoka mbali, wamewekwa kwa lorry, hlafulu wanaunganisha na wale watatu, wawili, wanasema tumeandika katika district hii, watoto sitini amd arobaini.

Nikimaliza, ningesema serekali iweze kusema ukweli, wasindganye watu, (laughter).

Mwisho ni ya kwamba katiba hii ambayo tumeandika leo, inaweza kurudia watu wa Cherangani kama leo hapa tupate kusikia Katiba hiyo? Asante, Mungu awabariki.

Com. Dr. Mosonik: Pengine swala lako tutajibu tukifunga. Tutarudia kujibu kwa ajili tulikuwa tumesema. Eliud Muturi.

Eliud Muturi: Kwa cmmisiners, nataka kuzungumza kidogo, mswli kidogo na ninaanza kwa rais: Ningetaka nguvu za rais zipunguzwe, na watu wote katika Kenya, wawe chini ya sheria moja. Mtu mkubwa, na mtu mdogo, mtu masikini, na mtu tajiri. Ningetaka president, awe akichaguliwa na 51% ya population ya Kenya, na makamu wake. Hapana makama kila wakati katolewa, wawe na tenure ya miaka yote pamoja.

Wafanyi kazi wote wa serikali, civil servants, top kama judges, permanent secretary, ambassadors wote wakiwa vetted by the parliament, na president anawateua baada ya parliament.

Tungetaka mambo ya foreign affair iwe ikifanywa na minister for foreign affairs. Minister awe na minister. tungetaka idadi ya minister ya Kenya, ipunguzwe katika Katiba, tuwe na kumi na saba kama French. Sisi sitajiri, na tunakuwa na minister karibu arobaine. Tungetaka hata utumishi ya president ya pesa, ya safari yake, ni sisi tunalipa kodi na ni lazima ziwe kama scheduled kama board zingine, zinapatiwa miaka ngapi. Hata ni lazima hata hiyo safari iandikwe ni ngapi, ambazo zitakuwa anatakiwa kuenda nje. Afadhali afanye kazi baada ya wao kutembea.

Tungetaka mwananchi wa Kenya awe na kipande ya Kenya, Kenya citizen lakini sasa kipande yangu ni Kenya na ni Mkikuyu, huyu ni Mjalu, huyu Mlughia, tungetaka iwe kipande moja ya Kenya.

Mimi niko kwa unitary government. Tunataka mtu yoyote wa Kenya, yake mahali popote katika Kenya, kwa sababu hata vita ikitoka atachukuwa bunduki, na kwenda kupigana.

Tunataka mtu yoyote wa Kenya awe loyal to the state, na awe tayari kulinda nchi, yake na kufania kazi nchi yake. Nataka mwananchi yoyote wa Kenya rudishe aliye na pesa hapa, iwe ndani ya Kenya, itumiwe katika Kenya, na akiwa yuko nje, huyo si mwananchi wa Kenya.

Citizenship: Tungetaka yule yoyote msichana akiolewa kule, anakwenda kuwa citizen wa kule, huyo anaolewa na mtu wa kenya anakuwa wa Kenya. Mtoto akizaliwa na mtu wa Kenya mwananume, ni mtoto wa Kenya, akizaliwa kule nje ni wa kule.

Kupiga kura: tungetaka tukipiga kura, watu wote wapige kura ya Kenya, kura moja kama vile tumepiga, na watu wote parliament wanapaiwa mshahara moja. Kwa hivyo wapatiwe watu wa kuwakilisha sawa sawa katika Kenya. Mtu mmoja, wengine sasa. Ikiwa ni kuraelfu hamsini watu wawe to, ikiwa ni councillor katika wadi wapatiwe the same number ya wapiga kura kwa sababu wanapatiwa mshahara pamoja.

Tenure of office ya president: Tungetaka akae term mbili peke yake, na aende na president akichaguliwa atoke kutoka miaka helahini na tano kuenda juu.

Elimu: Awe graduate na ambaye ana-track record na kazi amekwisha fanya hapo mbele ya kuonyesha ya kwamba, alikuwa amepita paa hiyo.

Tume zote za serikali, kama hii ya commissioner hii imechaguliwa, na hii ingine ya kura na zingine, zote zipatiwe katika sheria na ziwe zikichaguliwa graduate, ambao wao na integrity na maisha ambayo wako na heshima ya kazi yao wamekwisha fanya, na zaidi iwe watu wanahusika na sheria, ili waandikwe katika kufuata na sheria.

Wakati namaliza ningetaka katika gender. Tungetaka wamama, nataka vile tuwe pamoja wamama ni wengine kushinda wanaume katika state, lakini shida yao hawawezi, hawanauwezo wa kusimamia kura kwa sababu hawana pesa, na harassment ambayo inafanywa na youth, vyam, tungetaka kuwe na sheria kali kulinda harassment ya wakati wa uchaguzi, na tungetaka mjumbe akichaguliwa awe councillor amaliza mika tano. Pefection, hatuna katika dictation hi. Hiyo ni political corruption, na kusifanywe by election kw ajili ya mtu kuenda kuhama, akae parliament azungumze vile anataka, miaka tano, ikwishe, by-election inatumia pesa yetu nyingi, na watu wanaumizwa katika by-election, raia na hatunetaka kitu kama hiyo.

Tungetaka elimu ya Kenya, ipangwe kama ya zamani. Tulisoma na Carl Frnaxis, kitabu mbayo ilikuwa mihakama mazuri, na Durel, sasa vitabu vinaanguka vinabadilishwa bada y miaka tano inakuwa uneconomical kwa state, na uneconomical kwa wazazi. Tungetaka elmu, isingiliwe na siasa. Twataka waalimu walie na experts waendeshe kazi ya elimu.

Local government ipatiwe kazi ya kufanya hata mkiipatia federal system ni bure. Tunataka council kwa sababu, kila sehemu ya nchi, inatakiwa kupatiwa maendeleo hapo, na pesa wanayotoa kule watumie huko, na wwe wakipatiwa pesa zingine, na serikali kuu, na tuwe n hki y akunandika watu wao wakubwa, na kufua.

Wafanyi kazi: Tungetaka watu wote wafanyi kazi wa serikali, wajiondikishe mali zao, hata M.P. na councillor, na watu wanaiba mali ya serikali, wawe sheria moja ya kunyangwa kama wale wengine. Kw nini mnanyonga mtoto kwa kuiba kibeti y amam, ile ina only nappy, na mnaacha mtu ameandikwa kazi ya serikali, anaiba millions ana millions of money? Hapa councillor ningetaka wachaguliwe, kutoka standard 8, walio na kizungu, na Kiswahili.

Lugha yetu, iwe kiswahili, na international, iwe Kiingereza, kwa sababu ni lazima tu-communicate na watu wengine katika dunia.

Agriculture ndio ya Kenya ambayo inaweza kuandika watu wengi. Tungetaka budget iwekwe ya agriculture, na ma-corporate, kama corporate zilikuweco, K.C.C. zirudishiwe wananchi waziendeshe, na ili watu wengi wawze kuandikwa katika ministry of agriculture. Hata wataandika watu namna gani? Thank you commissioner nimezungumza zaidi.

Com. Dr. Mosonik: Asante.

Eliud Muturi: Lakini saa hakuna.

Com. Dr. Mosonik: Vile Mzee Muturi ame-summarise, bado tuna watu wachache, kama kila mtu angesema tu neno moja, tuatwasikia wote suuti kwa machine. Tafadhali M. sijui ni Macharia na Gichohi, it's the last time, just one word please.

M. Gichohi: (not clear)

Com. Dr. Mosonik: Nisha nasirika, nasikia iko mbele. One word each, so that they all get in the machine in terms of our presence here.

Michael Gichohi: Kwa majina, ni Michael Gichohi. Yangu ni machache kwa sababu mengi yamezungumzwa. Haswa ningezungumza kuhusu majeshi yetu ya Kenya. Majeshi wale wanalinda nchi, na polisi, na majeshi ya prison, hawa wanatakiwa wasisimamiwe na rais. Kuchaguliwa kama kwa mfano sasa kwa, kamani kamishna wa police,kuwe na tume ya kuchagua hoo watu, kuchunguza elimu yao na uwezo wao wa kufanya kazi, na wapewe nafasi ya kusimamia kazi yao kamili. Ndio ikiwa kutatokea makosa kidogo, huyo kamishna mwenyewe, anasmamishwa, ama anaambiwa ajiuzulu ndio kukiletwa mwingine, anachunguza maneno ya huyo mtu kwa njia nzuri. Kwa mfano, kama sasa, kamishna wa prison, inasemekana Nyeri kuna watu waliouwawa, na huyo mamishna bado ako kwa kazi.

Com. Dr. Mosonik: Tafadhali, unapendekeza?

Michael Gichohi: Sasa hiyo nimependekeza kuwe na tume ya kuchagua watu kama hawa.

Halafu ya pli ni hii neno kitu kidogo, katika Kenya. Hiyo ni ugonjwa imeshika watu wote wa Kenya, na hiyo ni kitu, ngumu sana kuondoa. Mimi ningependekeza, kuwe na lesson katika shule zote sha Kenya, watoto wetu wafunzwe hii hongo ni kitu mbaya. Ndio baada ya miaka ijayo wale watakaokuwa wa nyuma watakuwa wamejua kweli hongo si ktiu kizuri.

Tena, ningependekeza serikali iwe mbali na chama, kwa sababu, kama sasa kwa mfano, sasa kile chama ambacho kinatutawala, hata mbunge, hata nani anauwezo wa kufanya chochote viel anataka. Sasa serikali iwe mbali, wafanyi kazi wa serikali wawe mbali, na chama kiwe mbali.

Ya mwisho, katika Katiba, hiki kuna mahali nilisoma, maneno ya kadhi, huyu mkuu wa dini ya Kiislamu, walikuwa wanauliza kama inawezekana awe katika mahakama. Huyu awe akijishughulisha na maneno ya Kiislamu, lakini mahakama ya Kenya iwe inahudumia wananchi wa Kenya wote. Lakini sio kusema ati kuna Kadhi, ama Kristo, hapana. Watu wa Kenya wote wawe ni sawa. Asane sna.

Com. Dr. Mosnik: Asante, John Koech, dakika, 30 seconds please?

Interjection: Mbona umeturuka wengine tumeandikisha?

Com. Dr. Mosonik: Wapi? Nimeruka wapi?

Interjection: Isaack Biwot na mwengine hapa (not clear)

Com. Dr. Mosonik: Isaack Biwot ukiangalia number 103 is John Koech, number 104 Isaac Biwot, mimi siruki mtu. Please take me serious (laughter).

John Koech: Kwa majina naitwa John Koech mkaaji wa Kaplomai village. Mimi nina jambo moja, mbili, tatu, hivi, kushangisha katika Katiba ya Kenya, na katika Katiba mpya ya kurekebisha. Katiba ya kwanza kwa upande wangu, nataka irekebishwe kwa kusema kwamba, kwa sehemu mingi, unaweza kuta kuna M.P.s ambao wamechaguliwa na raia, kuna nominaed M.P.s na kuna civil servants. At times, unaweza kusikia kwa radio wakisema kwamba kuna pesa ambayo wamepitsha kwa bunge ku-develop, a constituency, in that particular area. So ningesema kwamba pesa kama hizo, wampatie, an elcted M.P. ambaye alichaguliwa na raia, sio kupatia nominated M.P.m ama D.c. ama any administrator.

Jambo la pili tena, ni issuing of title deeds. Tukiangalia kwamba katika uchumi yetu ya Kenya, saa zingine inaenda mpaka inaharibika tunasema ya kwamba, “uchumi imekuwa chini”, na ka upande wangu nataka kusema ya kwamba, jisi yakutengeneza uchumu kama huo, ni people should be encouraged to be very hard working. Issuing of title deeds, wapatiwe mtu ambaye ako hard working, kwa kufanya kazi. you are capable, with the ability of managing, 500 acre na ana-qualify ku-manage 500 acres, mpewe title deed ya 500 acres. Hakuna haja apewe 500 acres, na at long last you can manage only 10 acres, n huko mahali popote inakuwa forest. Hiyo ni kurdisha uchumi, yetu ikuwe chini.

Lidewise ningependa ku-encourage the government, waanze ku-assemble people to a certain particular place, halafu waangalie sehemu ambayo kuna ardhi, kuna rutuba wzilime, kama ni kulima mahindi, walime mahindi, na wazuze halafu the other money, wa-distribte to those people, kwa section ya meals, na kutumika ya basic needs. Likewise, kama wangeweza ku-assemble such people, waweke regualtional policies karibu na hao watu, halafu area zingine, wafanye ikuwe, very productive. For instance, kama sasa tuseme kwa Kericho, ikuwe very productive kwa kupanda chai, na watu wa Kericho waweke mahali, fulani halafu kuna magari ya kuwabeba, na kufanya kazi jioni wanarudishwa. itakuwa kitu nzuri, na itakuwa kazi ya kuinua uchumi yetu ya Kenya baada ya mwaka zengine.

After sometimes hatutalilia maneno ya I.M.F. na nini kwa msaada. Tutakuwa very productive, because Agriculture is the backbone of this country. Na specially...

Co. Dr. Mosonik: I would want each person to make only one point which nobody else has made, please eh? Sasa umalize yako.

John Koech: Sawa.

Com. Dr. Mosonik: Last.

John Koech: Thank you. Another points is that kuna section of tracing. Tunataka kwamba at times unaweza fanyiwa case ya rape case, I'm now talking about behaviours of dressing. We meet some other women they are dressing badly, which actually makes some other men to attract their...

Com. Dr. Mosonik: Are you recommending?

John Koech: I recommend

Com. Dr. Mosonik: Maxie or what?

John Koech: I recommend wavae nguo ambayo haiwezi kufanya some other malea to be ... (laughter)

Com. Dr. Mosonik: Hiyo imetosha.

John Koech: I hope you understand you people.

Com. Dr. Mosonik: Basi, Okay.

John Koech: Eeh, halafu...

Com. Dr. Mosonik: Sasa ikwishie hapo, please. Let us hear the next person.

John Koech: Thank you.

Com. Dr. Mosonik: Isaac Biwot. One point. Halafu Kamau Kinyanjui, halafu Meshak Nyasikira.

Isaac Biwot: Okay, asante sana. Kwa majina yangu naitwa Isaac Biwot, mimi ni mkaaji hapa kaplomaiz, nilizaliwa Kaplomai. Maoni yangu ya kwanza kama nachangikia katiba, maoni ya kwanza, kuhusikana na maneno ya Ministry of Health. Ningependelea heath kama doctor, ma-doctor wamekuwa watu wa kuwa na mahospitali. Ningependelea serikali alipe ma-doctor malipo mzuri, halafu madaktari wawache maneno ya kufungua mahospitali yao, clinics yao hizo. Imekuwa mtu, daktari wa hapa mtu anataka kufanyiwa operation ako kwa ile hospitali yake, ama usipopita kwa hospitali yake hawezi kuja kukupea matibabu mzuri kwa district. Atakupea matitabu nzuri kwa district kama anajua wewe ni mteja wake, kwa hivyo mtu asifanye biashara ingine akiwa anafanya kazi ya serikali ile inahusikana na hiyo biashara yake. Ama hata madawa vile unaweza patiwa district, mtu anaweza kuwa anakupleleka kwa biashara yake.

Haya ya pili, nakuja kwa mshahara ya mjumbe.

Com. Dr. Mosonic: Tulisema moja. Mshahara ya wajumbe tumesikia kila mtu akisema...

Isaac Biwot: Wacha tuwekw mbili, mbili pekee yake. Wa utaongeza ya mjimbe, mimi nitaweka moja ambayo inamaana kwangu, majimbo. Mi ningependelea sana majimbo sababu majimbo sisi wote tunajua story yetu na tunajua ni bado wapi.

Com. Dr. Mosonik: Okay.

Isaac Biwot: Kwa hivyo majimbo ikuwepo.

Com. Dr. Mosonik: Basum finished. Kamau Kinyanjui halafu Meshak Nyasikira. Kitu moja tu, tafadhali tutamaliza saa hii halafu tuombewe.

Meshak Nyasikira: Asante sana kwa nafasi hii. Mimi kenyenye nataka kupendekeza, serikali isaaidie mkulima. Mkulima

ameteseka sana.

Com. Dr. Mosonik: Na useme jina tena, urudie kwa hiyo machine.

Com. Dr. Mosonik: Kwa majina yangu naitwa Meshak Nyasikira. Napendekeza serikali isaidie mkulima sana kwa sababu serikali imewachilia mkulima kwa sababu, akilima mahindi, na watu wengine walaghai wanaleta mahindi kutoka nje. Sasa mkulima anakuwa kama mkulima ako bure kabisa.. Tunaomba serikali, itusaidie tena, kwa mbolea. Imewachilia mahindi amenyanyasa mkulima kabisa akiona hii kitu, anapandisha tena, akiona hii anapandisha tena. Sasa mkulima mpaka anapanda mahindi bila mbolea. Unaona, sasa ndio uchumi inanza kuzoroteka zaidi. Tena mkulima, walaghai wameleta mahindi kutoka nje na mkulima, ako na mahindi hapa. Sasa mkulima ameshindwa. Tunataka directors wachaguliwe, wa kusaidia mkulima, Ndio hilo pendekezo langu, napendekeza serikali isaidie wakulima. Tena kitu ya pili ni malize...

Com. Dr. Mosonik: Tumesema asante.

Meshak Nyasirika: ... kitu ya pili nimalize, watoto wakienda ma-secondary schools, kama ni m-S.D.A, Mcatholic, mtoto analazimishwa, aabudu siku ile secondary ameenda kama ni jumapili aabudu kama ni jumamosi, aabudi siku hiyo. Na mtoto kama ni m-S.D.A. je,. Anataka aabudu siku yake. Kama akiwa ni mmoja naonelea apewe siku yake, watoto wapewe siku ya kuabudu. Ndio naonelea hivyo, napendekeza hivyo. Asante sana.

Com. Dr. Mosonik: Asante. Salim Kifathi. Peter Lengech. Joseph Njuguna. Eliud Walufu. Mathayas Barasa. Paul Muragoli.

Paul Muragoli: Thank you honourable, Commissioner. My names are Paul Muragoli. My first proposal is that there should be a post of a Vice Attorney General, so that there can be fast dispensation of justice.

Another thing is that, there should be a law to escape the monopoly institutions especially the Kenya Power and Lighting Company. These are making Kenyans more poorer, than they are.

The third is that; the Provincial Administrator should be scrapped, because it is a flood gate of corruption in Kenya.

The last thing is that the Kenya Anti-corruption Authority, should be entrenched in the constitution. Thank you.

Com. Dr. Mosonik: Asante sana Mr. Paul Muragoli. William Yego.

William Yego: Majina zangu naitwa William Yego, na ningependekeza yafuatayo. Kwamba chiefs wawe retained, lakini wachaguliwe na wananchi vile mlolongo si ile ingine ya ku-apply.

Pili, kuwe na katiba ya kutoa elimu ya bure, kutoka nusery mpaka form 4.

Kwa mambo ya shamba; kusiwe na usawa, kwa kuwa na shamba, kati ya waume na wake.

Ingingine; Wakenya wawe na kiasi yoyote ya shamba, muradi tu alipate kwa njia ambayo ni haki as long as you can buy.

Ingingine, ni kwamba; Wanakenya wawe na shamba kila mahali popote pa Kenya.

Na ningependekeza serikali ya majimbo, kwa sababu yafuatayo-sehemu zingine kwa nchi hii yetu ya Kenya, we have 8 jimbos.

Com. Dr. Mosonik: Umesema majimbo hiyo ni sawa tafadhali.

William Yego: Sawa.

Com. Dr. Mosonik: Asante sana.

William Yego: Na ningependekeza pia iondolewe hii penalty ya... sheria ya kuna mtu akikosa.

Com. Dr. Mosonik: Yaani, hukumu ya kifo?

William Yego: Ya kifo

Com. Dr. Mosonik: Okay, abolish death penalty, thank you.

William Yego: Yes

Com. Dr. Mosonik: Asante sana. Tunakaribia kumaliza. Kiziah Onyango.

William Yego: Ningependekeza moja.

Com. Dr. Mosonik: Hiyo ilikuwa nini?

William Yego: President awe na all powers. Singependa kuona Rais ambaye hana nguvu (Laughter).

Com. Dr. Mosonik: Has all the power, eh?

William Yego: Yes.

Com. Dr. Mosonik: Okay.

William Yego: All the Presidents.

Com. Dr. Mosonik: Keziah Onyango, ameenda? Huyu Joseph Rono tulikuwa tumesikiza Joseph Rono, Huyu ni wa Box 266.

Interjection: Huyu ni mimi.

Com. Dr. Mosonik: Ah, wewe uko. Okay thank you.

William Yego: Mimi ningependa nitoe pendekezo langu katika tume hili, na singependa nirudie yale ambayo yamesemwa. Ya kwanza nikuwa, sisi kama wananchi wa Cherangani kwa mfano, tunapo chagua mbunge. Ni sharti tujue ni nani na vile vile anatoka wapi. Awe ni mtu ambaye tumemjua katika area hiyo, asiwe mtu ambaye anatoka mbali na sisi.

La pili, ni kuwa; mbunge ni sharti awe na ofisi katika kila division, ili awe akiwakilisha watu wake, au akitembelea watu wake.

Na kuhusu discipline ya wabunge katika bunge, ningependekeza ya kuwa mbunge akikosa nidhamu katika bunge, mshahara usimamishwe na ikuje katika.

Na kwa njia nyengine ni kwamba, ningependekeza pia kuhusu hili jambo la majimbo ni kuwa, tuiweke maanani, yaani mim ninapekeza hilo. Nafikiri sitaenda mengi kwa sababu ya wengine.

Com. Dr. Mosonik: Okay, S.K. Chepwoony, na Mr. Koskei.

William Yego: Asante sana Commissioners. Yangu ni machache tu. Mimi napendekeza, au napenda multi-party idumishwe, yaani vyama vingi.

Interjection: Jina lako?

David Koskei: David Kabarei Koskei. Nimesema multi-party idumishwe.

Nguvu za President zipunguzwe, na bunge ipewe nguvu zaidi.

Heshima ya katiba. Katiba iheshimiwe, ili kwamba, tusikuwe na kusema tunataka tusongeshe bunge au kupunguza.

Ya nne, katiba ya Kenya, iwe wazi kwa kila mtu, ajue asante.

Com. Dr. Mosonik: Asante kufikia hapo tume... Bwana Programme Officer, did you have any other list?

Hasan Mohammed: You can (not clear)

Com. Dr. Mosonik: Let's see. We are very tired. There was Wesley is it Kiplagat?

Hasan Mohammed: (Not clear)

Com. Dr. Mosonik: Let's just ...let us here. Excuse me, ngojeni tuna (David) Kiplagat huyu.

Hasan Mohammed: (Not clear)

Kiplagat Kirior: Thank you.

Hasan Mohammed: Ngojeni kwanza tusikizane. David Kosgei. Ndege Julius na walubengo. Sasa in that order eh? And everybody just 30 seconds, we'll finish in 2 minutes.

Kiplagat Kirior: My names are Kiplagat Kirior. I have the following. One the appointment of the minister, assistant minister, should be based on professional scale. The director also should be somebody with qualified skill in that area, and in case they make any mistake, they should resign.

There should be no interference of the head of state, in any of the duties of the above.

Registration of the political parties should be free and the party that register late with the same constitution, should be denied.

Federal system, I propose that freedom of speech to everybody.

Election should be done after every 5 years, and I propose that we go for election, with the need constitution.

Farming: The government should subsidize, the inputs for the farmers and these should be no importation of cereals and the government should buy all the cereals for the farmers. K.C.C. should be set immediately.

President should be literate and very popular 25% in every province and should be of sound mind, proved by a psychiatrist.

Com. Dr. Mosonik: Excuse me, have you finished?

Kiplaga Korir: Yes.....No. The vice-president should be 2, 1st vice-president, 2nd vice-president who is a woman.

Two, the MP: The MP should have an office in the constituency and they should not dictate their salaries. We should have a body that controls their salary.

Movement from political parties to another should be discouraged if you defect you lose your seat immediately and you don't contest.

Councillors should.....the waking up of the constituencies should be dictated by the population.

Councillors: The councillors should have offices in their wards, to serve the interests of the common mwananchi.

School: Free education upto form 2. Guideline for the school fees, from form 3, form 4 upto University. Categories of schools should be scrapped. All schools should be the same.

Employment should be done by institutions and pensions should be immediately you receive retirement letter.

Provincial administration: They should be paid by the government, these are the wazee ya mitaa.

Com. Dr. Koskei: Okay. Now Mr. David Koskei, just 30 seconds please. Ni sawa.

Ndege Julius: My names are Ndege Julius.

Com. Dr. Koskei: Where is David Koskei?

Ndege Julius: My names are Ndege Julius and my first proposal is that parliament's role in affecting constitution amendments need to be limited. It may only be allowed to alter the constitution but not change it.

Two, I propose that we have a reduced number of ministries, probably 15.

Three: Ministers should not be members of parliament. I wish I should have explained that.

The assistant ministers should be chosen from among parliamentarians.

Presidential elections, four to be delinked from parliamentary and civic elections. Presidential candidate to garner simple majority, 25% clause to be removed from every province.

Five, that due has been said, aspiring candidates.

Number six: Impediment of seating presidents should be allowed. The president should be impeached in case of misconduct.

Economic planning policies to be varied specific on particular projects to be carried out within our financial year. For example the year 2002, 2003 financial year we talk about farming of roads the year 2003 and four (4) we talk about provision of electricity like that.

Number eight: The idea of the A-G giving consent for prosecution, should be abolished to allow for quick dispensation of justice.

For the registration, it should be a continuous exercise. MPs should not decide their own salary.

Com. Dr. Mosonik: Asante sana. The last person is S. Walubengo.

S. Walubengo: I would propose a flexible constitution, that would have to suit the economy. Sylvester Walupengo sir. I would propose a national referendum, any time we are having an economic crisis, or an international crisis.

I would also propose, that in the constitution, in the event of the office of the head of state falling vacant we would wish to have

the speaker, taking over those duties for the specified 90 days.

I would propose that, if there were any policies, that emanated from party struck work independence on indigenous and lead to the misrule, that turned into tribal benefits, let them be scrapped if there were any such.

I would also propose, that the national way of collecting taxes has been so questionable, that the thing that would have helped us improve on the economic standing of the country, has been ignored. We are having taxation restricted to very few people, and there have too many ticks, the nation is having. Thank you sir.

Com. Dr.Mosonik: Asanteni sana. Kufikia hapo, tumemaliza kikao chetu rasmi cha leo na ya kurekebisha katiba ya Kenya. Ninapenda bwana district co-ordinator, pengine aseme meno moja, ama mbili.

District Co-ordinator: Asante sana commissioners kwa siku moja ambayo imekuwa ndefu sana. Tungepende kuwashika sana, kwa kujitolea kwenu na kujitolea kabisa kwa kufanya kazi hii. Pia ningependa kuchukuwa nafasi hii kushukuru kanisa la St. Andrews A.C.K. Church, kwa kutupa nafasi hii. Tunajua labda watu wamekanyaga mana pale nje, wamefanya nini, lakini tunashukuru sana, kwa usaidizi wenu. Kwa kumaliza kabisa, ingelipenda kutoa nafasi hii, kwa mama Bi-Kimani aliyetufungulia kwa maombi, atufungie ka maombi haya, ili kazi yetu iwe imemalizika rasmi. Karibu Bi Kimani.

Bi-Kimani: Tusimame na tuamini. Baba mwenyezi, tunataka kutuina, na kukusifu, kwa sababu umekuwa mwema kwetu mchana kutwa tangu tulipokaa mahali hapa. Tulianza nawe, na tukakuomba ya kwamba kanze nazi, uenende nasi, na ukumalizie nasi, na sasa mungu umemaliza nasi, tunataka tukushukuru hata kwa commissioners, na wale wote walioandamana nao, na wanaohusika kwa mpango huu, watakapokuwa wakiondoka mahali hapa, Utawapa amani na safari njema, mahali watakapoenda. Mbinu zote za muovu shetani, na hila zake zote, za kutaka kuangamiza roho za watu wako, ziweze kupotelea mbali, na watafikapo salama mahali wanapoenda, tutakapo sikia walimaliza kazi yao vizuri, na wakarudi Nairobi salama salimini, tutaliinua jina lako na kusema ni asante. Asante Mungu wetu, kwa sababu ulisikia maombi yetu, hata tukakuuliza ya kwamba pengine ufunge mvua isinyshe, ili watu waziweza kuhangaika, na ukafanya hivyo Mungu wetu, na hivyo tunakushukuru, na kukinua jina lako, na hasa Mungu hata tutakuwa na chakula kidogo, kwa ajili ya wageni, utakapo kitumia Mungu, utuweza kuwasaidia meli yao, kwa ajili ya kazi ambayo wanafanya. Tunaomba hayo tukijua umesikia maombi yetu, na utazidi kutubariki, katika jina la Yesu Kristu aliye bwana, na mwokozi wetu.

Audience: Amina

Bi-Kimani: Asante